# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

# KIONGOZI CHA UTEKELEZAJI WA MWONGOZO WA UENDESHAJI NA VIWANGO KATIKA ELIMU YA AWALI TANZANIA BARA

**2023**

KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 1 15/04/2023 15:39

© Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

Toleo la kwanza, 2023

ISBN: 978–9987–09–543–8

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,

Mtaa wa Afya - Mtumba,

S.L.P. 10,

**40479 Dodoma.**

Simu: +255 26 296 3533

Baruapepe: info@moe.go.tz

Tovuti: www.moe.go.tz

Mwongozo huu utarejelewa kama:
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. (2023). Kiongozi cha Utekelezaji wa Mwongozo wa Kitaifa wa Uendeshaji na Viwango katika Elimu ya Awali. Dodoma.

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kutafsiri, kurudufu, kupiga chapa, wala kutoa andiko, hili kwa namna yoyote ile bila idhini ya Kamishna wa Elimu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

## YALIYOMO

**Dibaji**........................................................................ v

**Shukurani**........................................................................ vi

**Orodha ya Majedwali**.................................................. xi

**Vifupisho**........................................................................ xiii

**SEHEMU YA KWANZA**

**UTANGULIZI**........................................................... 1

1.1 Usuli........................................................................ 1

1.2 Sababu za Kuandaa Kiongozi cha Utekelezaji wa MUVEA........................................................ 2

1.3 Mitazamo Mbalimbali kuhusu Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto...................... 4

1.4 Umuhimu wa KUMUVEA................................... 9

1.5 Malengo ya KUMUVEA .................................... 11

1.6 Walengwa wa Kiongozi.................................... 12

**SEHEMU YA PILI**

MAZINGIRA WEZESHI KATIKA MALEZI, MAKUZI NA MAENDELEO YA AWALI YA MTOTO.. 13

2.1 Utangulizi........................................................... 13

2.2 Uwekezaji katika Mazingira ya Ujifunzaji.......... 18

2.3 Upatikaji wa Huduma Stahiki............................ 38



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 3 15/04/2023 15:39

**SEHEMU YA TATU**

UPIMAJI WA MATOKEO YA UJIFUNZAJI............... 83

3.1 Utangulizi........................................................ 83

3.2 Namna ya Kupima Viwango vya Utendaji........ 84

3.3 Tathmini ya Ubora wa Shule............................ 115

3.4 Ziara ya Uthibiti Ubora wa Shule...................... 115

**SEHEMU YA NNE**

UFUATILIAJI NA TATHIMINI YA UENDESHAJI WA ELIMU YA AWALI .................................................... 119

4.1 Utangulizi........................................................ 119

4.2 Matokeo ya Tathmini ya Ubora........................ 120

4.3 Viashiria vya Ufanisi....................................... 129

**Marejeleo**............................................................ 131

# DIBAJI

Utekelezaji wa sera, sheria, kanuni, na miongozo ya kielimu katika ngazi husika huhitaji nyenzo mbalimbali ili kuwawezesha wadau kuitekeleza kwa ufanisi na kufikia malengo yaliyotarajiwa. Serikali imeidhinisha utekelezaji wa "Mwongozo wa Kitaifa wa Uendeshaji na Viwango katika Elimu ya Awali (MUVEA)". Kutokana na mwongozo huu, Kiongozi cha Utekelezaji wa Mwongozo wa Uendeshaji na Viwango katika Elimu ya Awali (KUMUVEA) kimeandaliwa ili kuwawezesha wadau kutekeleza mwongozo huo kwa ufanisi. Aidha, kiongozi kinawawezesha watekelezaji wa Mwongozo kuhakikisha kwamba kunakuwa na viashiria vya kuonesha kuwa utekelezaji umefanyika.

Matumizi ya kiongozi hiki yanatarajiwa kurahisisha utekelezaji wa MUVEA kwa lengo la kuwaandaa vyema watoto wa Elimu ya Awali ili kuwa na Mtanzania aliyeelimika katika Sayansi na Teknolojia kwa maendeleo yake na taifa kwa ujumla. Aidha, kiongozi hiki kitawezesha utoaji wa huduma toshelevu katika Elimu ya Awali kwa kuzingatia mahitaji ya kila mtoto kufikia mabadiliko ya jumla kiakili, kimwili, kijamii, na kimaono.



Prof. Carolyne I. Nombo

**Katibu Mkuu,**

**Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia**



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 5 15/04/2023 15:39

## SHUKURANI

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (WyEST) inatambua na kuthamini mchango muhimu wa washiriki waliofanikisha uandishi wa Kiongozi cha Utekelezaji wa Mwongozo wa Uendeshaji na Viwango katika Elimu ya Awali kuwezesha utekelezaji wa MUVEA kwa kuhakikisha kwamba viashiria vya mabadiliko vimefikiwa inavyotakiwa.

WyEST inatoa shukurani za dhati kwa mchango uliotolewa na wataalamu wenye uzoefu mkubwa walioandaa kiongozi hiki. Aidha, kwa nafasi ya pekee watatajwa baadhi ambao walihusika moja kwa moja na uandaaji, utayarishaji na ukamilishaji wa kiongozi hiki kama ifuatavyo:

| Na. | Mshiriki | Taasisi anayotoka | Jukumu lake |
|---|---|---|---|
| 1 | Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa | WyEST | Mtaalamu |
| 2 | Venance Manori | WyEST | Mshauri |
| 3 | Suzana Nussu | OR-TAMISEMI | Mshauri |
| 4 | Hawa J. Selemani | WyEST | Mratibu na Mtaalamu |
| 5 | Dkt. Cosmas Mnyanyi | CKHT | Mtaalamu Mwelekezi |

| Na. | Mshiriki | Taasisi anayotoka | Jukumu lake |
|---|---|---|---|
| 6 | Dkt. Wilbaforce Meena | Haki Elimu | Mhariri |
| 7 | Dkt Pambas Tandika | UDOM | Mwenyekiti |
| 8 | Dkt. Fortunata Pembe | UDOM | Katibu na Mhariri |
| 9 | Modesta Ng'aida | CCU Butimba | Mwandishi |
| 10 | Grace Shileringo | WyEST | Mhariri |
| 11 | Timoth Zumbi | WyEST | Mchapishaji |
| 12 | Edson Mapunda | WyEST | Mchapishaji |
| 13 | Kilen Malugu | Mstaafu | Katibu Muhtasi |
| 14 | Sengi Gibson | WyEST | Katibu Muhtasi |
| 15 | Joanitha Mchunguzi | WyEST | Katibu Muhtasi |
| 16 | Davis Gisuka | Children in Crossfire | Mwandishi |
| 17 | Faraji Paraga | Children in Crossfire | Mwandishi |
| 18 | Mussa Swila | CCU Mhonda | Mwandishi |



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 7 15/04/2023 15:39

| Na. | Mshiriki | Taasisi anayotoka | Jukumu lake |
|---|---|---|---|
| 19 | Noreen Kwezi | CCU Nachingwea | Mwandishi |
| 20 | Winifrida Mlope | CCU Nachingwea | Mwandishi |
| 21 | Bakari Chambo | CCU Singachini | Mwandishi |
| 22 | Aniset Temba | CCU Singachini | Mwandishi |
| 23 | Annet Poul | CCU Mpuguso | Mwandishi |
| 24 | Lilian Charles | CCU Mandaka | Mwandishi |
| 25 | Vidda Ngowi | TET | Mwandishi |
| 26 | Joyce Chamhulo | TET | Mwandishi |
| 27 | Francisca Tarimo | TET | Mhariri |
| 28 | Nuru J. Mwevira | Uthibiti Ubora – Morogoro | Mwandishi |
| 29 | Prof. Aldin Mutembei | CKD | Mtaalamu Mwelekezi |
| 30 | Dkt. Titus Mpemba | CKD | Mhariri |



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 8 15/04/2023 15:39

| Na. | Mshiriki | Taasisi anayotoka | Jukumu lake |
|---|---|---|---|
| 31 | Lujeko Mwinuka | Uthibiti Ubora kanda DSM | Mwandishi |
| 32 | Clarence Mwinuka | Mstaafu | Mtaalamu na Mhariri |
| 33 | Madina Kemilembe | Mstaafu | Mhariri |
| 34 | Revocatus Kundi | Mstaafu | Mtaalamu na Mhariri |
| 35 | Ally  Swalehe | TAMISEMI | Mhariri |
| 36 | Salvatori Alute | TAMISEMI | Mwandishi |
| 37 | Riaz Abed | TAMISEMI | Mhariri |
| 38 | Maimuna H. Amour | WyEST | Mtaalamu na Mhariri |
| 39 | Hanifa Mponji | Shule ya Msingi Mlimani (DSM) | Mtaalamu |
| 40 | Rechel Kakulima | Shule ya Awali na Msingi Tusiime | Mtaalamu |



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 9 15/04/2023 15:39

| Na. | Mshiriki | Taasisi anayotoka | Jukumu lake |
|---|---|---|---|
| 41 | Hassan Masoud | Shule ya Awali na Msingi Kansenene (Bukoba) | Mtaalamu |
| 42 | Venance N. Manori | WyEST | Mtaalamu |
| 43 | Peter M. Mbute | TET | Msanifu |

Vilevile shukurani zinatolewa kwa USAID katika mradi wa Jifunze Uelewe, Shirika la Watoto -Children in Crossfire katika mradi wa Watoto Wetu Tunu Yetu, HakiElimu na Plan International kwa kushirikiana nasi bega kwa bega katika kufanikisha uandishi wa kiongozi hiki.

Shukurani za pekee ziende kwa “Global Partnership for Education kupitia Mradi wa Kukuza Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu uitwao “Literacy and Numeracy Education Support kwa ufadhili wao uliofanikisha kufanyika kwa utafiti, uandaaji wa ripoti na uandishi wa KUMUVEA pamoja na zana za upimaji.



Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
Kamishna wa Elimu,
**Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia**



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 10 15/04/2023 15:39

## ORODHA YA MAJEDWALI


**Jedwali Na. 1:** Hatua za Ukuaji na Uchangamshi wa Awali wa Mtoto.............................14

**Jedwali Na. 2:** Kumtambua Mtoto mwenye Changamoto za Uoni.........................44

**Jedwali Na. 3:** Kumtambua Mtoto mwenye Changamoto za Ualibino................... 47

**Jedwali Na. 4:** Kumtambua Mtoto mwenye Ukiziwi.. 42

**Jedwali Na. 5:** Vifaa na Matumizi katika Kumtambua Mtoto mwenye Uziwi..........................50

**Jedwali Na. 6:** Kumtambua Mtoto mwenye Changamoto za Ukiziwi Kutoona........52

**Jedwali Na. 7:** Kumtambua Mtoto mwenye Ulemavu wa Akili............................................ 55

**Jedwali Na. 8:** Kumtambua Mtoto mwenye Usonji............................................... 58

**Jedwali Na. 9.** Kumtambua Mtoto mwenye Kipaji na Kipawa....................................... 60

**Jedwali Na. 10:** Kumtambua Mtoto mwenye Changamoto za Kiafya..................... 62

**Jedwali Na. 11:** Kumtambua Mtoto mwenye Changamoto za Kijamii, Kihisia na Kitabia......................................... 65

**Jedwali Na. 12:** Kumtambua Mtoto mwenye Changamoto za Kipekee za Ujifunzaji..67
**Jedwali Na. 13:** Kumtambua Mtoto mwenye Ulemavu wa Viungo..........................................69
**Jedwali Na. 14:** Kumudu Stadi za Awali za Kuhusiana. .. ......................................................... 91
**Jedwali Na. 15:** Kumudu Stadi za Awali za Lugha na Mawasiliano................................ 98
**Jedwali Na. 16:** Kumudu Stadi za Kutunza Afya....... 104
**Jedwali Na. 17:** Kumudu Stadi za Kutunza Mazingira..107
**Jedwali Na. 18:** Kumudu Stadi za Kisanii, Ubunifu na Michezo.................................... 109
**Jedwali Na. 19:** Kumudu Stadi za Kutumia Stadi za Awali za Kihisabati, Kisayansi na TEHAMA....................................113



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 12 15/04/2023 15:39

# VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| **BEST** | Basic Education Statistic in Tanzania |
| **CCU** | Chuo cha Ualimu |
| **CKD** | Chuo Kikuu cha Dar es salaam |
| **CHT** | Chuo Kikuu cha Huria Tanzania |
| **EA** | Elimu ya Awali |
| **GPE** | Global Partnership Education |
| **KKK** | Kusoma, Kuandika, Kuhesabu |
| **KUMUVEA** | Kiongozi cha Utekelezaji wa Mwongozo wa Uendeshaji na Viwango katika Elimu ya Awali |
| **LANES** | Literacy and Numeracy Education Support |
| **MUVEA** | Mwongozo wa kitaifa wa Uendeshaji na Viwango katika Elimu ya Awali |
| **MJUKUM** | Mtazamo Jumuishi wa Ujifunzaji Kuzingatia Utendaji wa Mtoto |
| **MMEM-I, II** | Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi |
| **OR-TAMISEMI** | Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 13 15/04/2023 15:39

| | |
|---|---|
| **TEHAMA** | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| **TET** | Taasisi ya Elimu Tanzania |
| **UKIMWI** | Upungufu wa Kinga Mwilini |
| **UNICEF** | United Nations Children's Fund |
| **UWAWA** | Umoja wa Wazazi na Walimu |
| **JZK** | Jumuiya za Kujifunza |
| **WyEST** | Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia |
| **VVU** | Virusi vya UKIMWI |



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 14 15/04/2023 15:39

# SEHEMU YA KWANZA

## UTANGULIZI

### 1.1 Usuli

Tangu ulipotangazwa Mwaka wa Kimataifa wa Mtoto Mwaka 1979, Serikali ya Tanzania imekuwa na mipango ya maendeleo ya kuboresha mazingira ya ujifunzaji na ufundishaji kwa watoto wa Elimu ya Awali. Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (WyEST), kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI, pamoja na wadau wengine, imefanya maboresho makubwa katika Mpango wa Maendeleo ya Elimu Msingi (MMEM I na II). Mipango imelenga kutoa elimu bora kwa watoto wote ili kukidhi mahitaji yao. Mambo yaliyoboreshwa ni pamoja na majengo na uandikishaji wa watoto kufikia mwaka 2021 (BEST, 2020/ 2021).

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, kwa kushirikiana na UNICEF, ilifanya utafiti katika mikoa ya Kagera, Geita, Dar es Salaam, Lindi, Njombe, na Songwe ili kuona uendeshaji na ufikiaji wa viwango vya utoaji wa Elimu ya Awali. Utafiti huo ulibaini kuwapo kwa changamoto kadhaa za utoaji wa Elimu ya Awali na kupendekeza kuweka mikakati ya kuboresha upatikanaji wa fursa ya elimu bora ya awali kwa watoto wote.



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 1 15/04/2023 15:39

Mwongozo wa Kitaifa wa Uendeshaji na Viwango katika wa Elimu ya Awali Tanzania (MUVEA) umeandaliwa kama moja ya nyenzo za kuwezesha kufikia ubora wa elimu. Aidha, viashiria vya ubora katika utoaji wa Elimu ya Awali vimebainishwa ili kuwasaidia walengwa kupata matokeo ya utoaji wa huduma kwa maendeleo ya ujifunzaji na ukuaji wa mtoto. Vilevile, Mwongozo umeweka mazingira wezeshi katika utoaji wa Elimu ya Awali ambayo ni msingi wa kukuza stadi mbalimbali, zikiwamo za kihisabati, lugha na mawasiliano, kuhusiana, michezo na sanaa, utunzaji wa afya na utunzaji wa mazingira. Stadi hizi zitasaidia kukuza stadi za karne ya 21 za mawasiliano, ushirikiano, fikra tunduizi, na ubunifu. WyEST imeandaa Kiongozi cha Utekelezaji wa Mwongozo wa Uendeshaji na Viwango katika Elimu ya Awali (KUMUVEA) ili kuwezesha wadau kutekeleza MUVEA kwa namna itakavyosaidia kukidhi malengo ya utoaji wa elimu bora.

### 1.2 Sababu za Kuandaa Kiongozi cha Utekelezaji wa MUVEA

Kiongozi cha Utekelezaji wa MUVEA kimeandaliwa ili kuwasaidia wadau kukidhi mahitaji ya utekelezaji wa Mwongozo wa Kitaifa wa Uendeshaji na Viwango katika Elimu ya Awali (MUVEA). Kwa sababu hiyo, kinaelekeza wadau wa elimu kutekeleza majukumu yao ili kufikia viwango vilivyotajwa katika MUVEA.



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 2 15/04/2023 15:39

Kiongozi hiki kinashughulikia maeneo makuu matano ambayo ni:

i. Taarifa za awali za Mwongozo;
ii. Mazingira wezeshi yanayotakiwa kuandaliwa vema kumwezesha mtoto kukua kimaono, kiutendaji, kijamii na kihaiba;
iii. Mafunzo endelevu ya walimu kazini yanayoendelea kumjenga mwalimu kitaaluma na kitaalamu akiwa kazini;
iv. Upimaji wa matokeo ya ujifunzaji ili kubaini kiwango kilichofikiwa kutokana na mchakato wa ujifunzaji; na
v. Ufuatiliaji na tathmini katika Elimu ya Awali.

Serikali inatumaini kwamba walengwa watakaotumia kiongozi hiki wataweza kujenga mazingira rafiki ya ujifunzaji wa mtoto wa Elimu ya Awali. Mazingira hayo ni pamoja na mazingira ya kisaikolojia, mazingira ya kiutendaji yenye miundombinu na vifaa, na mazingira ya kiuhusiano yanayohusisha Ushirikiano wa Wazazi na Walimu (UWAWA) kuendeleza utayari wa mtoto katika kujifunza kufikia makuzi na maendeleo timilifu kiakili, kimwili, kijamii, kihaiba na kihisia.

Mchakato wa ujifunzaji ni lazima uanze na maandalizi ya ufundishaji, ambayo ufanisi wake unategemea zaidi umahiri wa mwalimu katika kuchambua mtaala, kutumia



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 3 15/04/2023 15:39

mbinu shirikishi kuwezesha ujifunzaji kwa kuzingatia mahitaji ya kila mtoto. Umahiri wa mwalimu wa Elimu ya Awali umesisitizwa katika kiongozi hiki, ambapo mwalimu atatakiwa kubainisha vikwazo vinavyokwamisha ujifunzaji, vikiwamo vya kiusalama, kijiografia na kimaumbile ili kutoa afua stahiki kwa kushirikisha wadau wengine wakiwamo wazazi na jamii. Maandalizi ya miongozo na viongozi vinavyolenga kutoa maelekezo ya namna ya kutoa huduma kwa kuzingatia viwango ni lazima viongozwe na mitazamo iliyopo. Mitazamo imegawanywa katika makundi matatu ambayo ni mtazamo wa kimataifa, mtazamo wa kikanda na mtazamo wa kitaifa:

## 1.3 Mitazamo Mbalimbali kuhusu Malezi, Makuzi NA Maendeleo ya Awali ya Mtoto

Kiongozi hiki kimeandaliwa kwa kuzingatia mitazamo ya kimataifa, kikanda na kitaifa.

### 1.3.1 Mitazamo ya Kimataifa

Kiongozi hiki kimeandaliwa ili kuhakikisha kunakuwa na mpango wa upatikanaji wa huduma bora kwa maendeleo ya watoto wote.

Kiunzi cha Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto cha 2018 kimesisitiza huduma jumuishi ili kumwendeleza mtoto katika majazi matano, ambayo ni:



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 4 15/04/2023 15:39

i. Maendeleo ya lugha na ufahamu wa awali wa kusoma na kuandika;
ii. Utambuzi na maarifa zikiwamo stadi za awali za Hisabati na Maendeleo ya Sayansi na Teknolojia;
iii. Makuzi ya kimwili;
iv. Makuzi ya kihisia na kijamii; na
v. Uendelezaji wa sanaa na michezo

Tafiti nyingi katika vipindi tofauti zinathibitisha kuwa msingi imara unatakiwa kujengwa katika miaka ya awali ya mtoto na kwamba huu ndiyo wakati muhimu wa kuwekeza kwenye maisha ya mwanadamu. Mtaalamu Maria Montesori, Jean Piaget, na Lev Vygotsky wanashauri kuwa, katika miaka ya mwanzo, mtoto anatawaliwa na akili ya kufyonza kila kitu na yupo tayari kujifunza iwapo ataandaliwa mazingira yanayochochea ujifunzaji kwa vitendo zaidi. Aidha, mtoto hulelewa na jamii nzima inayomzunguka. Kwa hiyo, michezo ina nafasi kubwa ya kujenga utambuzi kutoka hatua ya chini kwenda hatua ya juu ya utambuzi wake.

### 1.3.2 Mtazamo wa Kikanda

Mkataba wa Afrika umesisitiza kuwa watoto wanaendelezwa kimwili, kiakili na kukuza vipaji ili waweze kufikia utimilifu wao. Mambo muhimu yanayopaswa kuboreshwa ni pamoja na huduma



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 5 15/04/2023 15:39

za afya, elimu, lishe bora, makazi, malazi, malezi bora, mazingira rafiki ya ukuaji wao, ulinzi na usalama. Vilevile, msisitizo umewekwa katika haki za mtoto mwenye ulemavu kupata uangalizi maalumu na ulinzi wakati wote wa ukuaji wake bila kubaguliwa na kuhakikisha upatikanaji wa huduma rafiki na stahiki kwa watoto wenye mahitaji maalum.

### 1.3.3 Mtazamo wa Kitaifa

Serikali ya Tanzania inasisitiza suala ya malezi makuzi, na maendeleo ya awali ya mtoto lisimamiwe na sekta tofauti kama vile sekta ya afya, maendeleo ya jamii na elimu kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ambayo inatambua watoto na kuheshimu haki za watoto, wakiwamo watoto wenye mahitaji maalumu. Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 1995 inatambua Elimu ya Awali kuwa ni miongoni mwa elimu rasmi inayohitajika kutolewa nchini.

Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 imeweka tamko namba 3.1.2 linalosisitiza utoaji wa Elimu ya Awali kwa watoto wote wenye umri kuanzia miaka 3 hadi 5 kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja. Aidha, Sheria



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 6 15/04/2023 15:39

ya Mtoto Namba 21 ya mwaka 2009 inasisitiza mtoto kuendelezwa kimwili, kiakili, kijamii, na kihisia na kuhakikisha kuwa maslahi ya mtoto yanapewa kipaumbele katika utoaji wa huduma stahiki. Vilevile, kanuni za vituo vya kulelea watoto wadogo mchana na watoto wachanga zinasisitiza makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto na umuhimu wa malezi changamshi ya awali katika ujifunzaji.

**Taasisi ya Malezi na Maendeleo ya Mtoto Tanzania Visiwani**

Programu Jumuishi ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Mtoto kwa Tanzania Visiwani kwa miaka zaidi ya 30 imekuwa ikitolewa kwa kufuata mtazamo wa madrasa katika malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto kwa kufanya yafuatayo:

i. Ushiriki wa Jamii: Jamii hushirikishwa katika makuzi ya awali ya mtoto kwa kuhamasishwa kutafuta rasilimali, kujenga miundombinu na kushirikisha uongozi wa serikali za mitaa;

ii. Mafunzo ya walimu: kuna kozi tofauti zinazotolewa katika vyuo vya walimu kwa kuzingatia sifa maalum kulingana na kozi husika pamoja na mafunzo ya walimu waliomo kazini;

iii. Ushiriki wa wazazi: Wazazi hushirikishwa katika



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 7 15/04/2023 15:39

makuzi na ujifunzaji wa watoto wao, ikiwamo kutafuta na kutengeneza vifaa vya kufundishia na kujifunzia watoto;

iv. Mazingira ya skuli: Mazingira ya skuli yaliyo rafiki kwa watoto kujifunzia yanahusisha mazingira ya ndani, mazingira ya nje na miundombinu katika skuli za maandalizi; na

v. Mtaala jumuishi: mtaala unaowapa nafasi watoto wote kujifunza, unaozingatia makuzi ya jumla ya mtoto, mbinu shirikishi za ufundishaji na ujifunzaji pamoja na vifaa vya kufundishia na kujifunzia vya gharama nafuu.

Programu ya Malezi Jumuishi kwa Tanzania Bara ya mwaka 2022 imeandaliwa kutokana na kanuni za mfumo wa malezi jumuishi katika utoaji wa huduma za malezi kwa watoto. Mfumo huu umezingatia hali halisi nchini katika kushughulikia mahitaji ya malezi jumuishi ili kuleta matokeo chanya. Programu jumuishi imelenga pia katika kutekeleza Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014.

Sera hii imerasimisha Elimu ya Awali kuwa ya lazima kwa watoto wa rika lengwa wenye umri wa miaka 3 - 5 kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja. Sera hiyo inazingatia Tamko la Umoja wa Mataifa kuhusu Haki ya Mtotola mwaka 1989 ambalo linasisitiza haki za mtoto zinazojumuisha huduma bora za afya, elimu, ulinzi,

kutobaguliwa na usalama. Vilevile, Tamko la Kimataifa la Jomtieni kuhusu Elimu kwa Wote la mwaka 1990 linasisitiza umuhimu wa ufundishaji na ujifunzaji wenye ufanisi kwa mtoto. Vilevile, Azimio la Elimu kwa Wote la mwaka 2000 linasisitiza kuwa mahitaji ya kila mtoto lazima yazingatiwe.

Matamko na miongozo inayolenga utekelezaji wa utoaji wa Elimu ya Awali vinatakiwa kupewa umuhimu wa kipekee kiutekelezaji ili kuhakikisha kwamba watoto wote wanapata elimu bora inayokidhi mahitaji yao. Utekelezaji huu unahitaji kiongozi cha kutekeleza MUVEA kufikia malengo yaliyowekwa. Kiongozi hiki pia kinasisitiza katika kuifanya Elimu ya Awali nchini kufuata **Mtazamo Jumuishi wa Ujifunzaji Kuzingatia Utendaji wa Mtoto (MJUKUM)**. Mtazamo huu umelenga kumwezesha mtoto kucheza na kujifunza dhana mbalimbali zinazomwezesha kujenga umahiri katika nyanja za kiakili, kimwili, kijamii, kimaono na kihisia ili kufikia utimilifu wake.

## 1.4 Umuhimu wa KUMUVEA

Mazingira wezeshi katika utoaji wa Elimu ya Awali ni muhimu ili kupata utimilifu wa huduma kwa watoto. Kiongozi hiki kinatoa msisitizo katika vipaumbele vya mazingira wezeshi yanayojumuisha: uwapo wa sera, sheria na miongozo inayotoa kipaumbele katika upatikanaji wa huduma stahiki kwa watoto wote; kutenga rasilimali za kutosha ili kutoa afua toshelevu; kuwapo kwa uratibu wa



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 9 15/04/2023 15:39

masuala ya watoto kuanzia ngazi ya taifa hadi jamii pamoja na ushirikishwaji wa jamii katika kutoa huduma za Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (MMMAM). Kwa kuwa Elimu ya Awali imejikita katka malezi shirikishi, yanayohitaji ushiriki wa wazazi, walezi, walimu na jamii kwa ujumla, Kiongozi cha Utekelezaji wa MUVEA kinatoa maelekezo stahiki kwa wadau wote ili waweze kushiriki kikamilifu katika utoaji wa huduma stahiki kwa mtoto kulingana na mahitaji yake. Mambo muhimu ya kuzingatia ni pamoja na:

i. Kuimarisha mifumo ya utoaji huduma za MMMAM;
ii. Kuongeza wigo wa upatikanaji wa huduma stahiki zilizoratibiwa vyema;
iii. Kujenga uwezo wa watoa huduma za MMMAM kuwa na mtazamo chanya; na
iv. Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa program za MMMAM.

Taarifa ya ufuatiliaji wa hali halisi ya utekelezaji wa Elimu ya Awali ilibainisha kuwa kukosekana kwa MUVEA kulisababisha huduma hizi kutolewa bila kuzingatia viwango vya ubora. Kiongozi cha KUMUVEA kitatumika kama nyenzo ya utekelezaji kwa kutoa maelekezo ya nini kifanyike kufikia utekelezaji wa viashiria mbalimbali vya ubora wa Elimu ya Awali. Aidha, utekelezaji wa kiongozi hiki utawawezesha wadau wa Elimu ya Awali kuwa na



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 10 15/04/2023 15:39

mikakati endelevu ya kuwekeza katika mazingira ya kutoa fursa kwa watoto wote ili kupata elimu bora.

## 1.5 Malengo ya KUMUVEA

Kiongozi hiki kina lengo kuu moja na malengo mahsusi manne.

### 1.5.1 Lengo Kuu

Lengo kuu la kiongozi ni kuweka bayana utaratibu na maelekezo ya utekelezaji wa MUVEA ili kuboresha utoaji wa Elimu ya Awali kwa kuzingatia viwango vya ubora vinavyokubalika kitaifa na kimataifa.

### 1.5.2 Malengo Mahususi

Malengo mahsusi ya kiongozi hiki ni:

i. Kutoa maelekezo sahihi ya namna ya kufikia viwango stahiki vya utoaji wa Elimu ya Awali;

ii. Kutoa maelekezo stahiki yatakayosaidia wadau kuwekeza katika kuboresha mazingira ya utoaji wa Elimu ya Awali;

iii. Kuwezesha wadau wa Elimu ya Awali kuzingatia taratibu sahihi katika kuendesha na kutoa huduma stahiki; na

iv. Kutoa maelekezo sahihi yatakayosaidia



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 11 15/04/2023 15:39

kufanya upimaji, ufuatiliaji na tathmini na kutunza kumbukumbu.

### 1.6 Walengwa wa Kiongozi

Watumiaji wa kiongozi hiki ni wadau wote wanaotoa huduma ya Elimu ya Awali, wakiwamo watafiti, wawezeshaji, viongozi na maafisa wa Serikali katika ngazi ya WyEST, OR-TAMISEMI, wizara za kisekta zinazohusika na malezi na makuzi ya mtoto, idara na taasisi zake, mikoa, halmashauri, asasi zisizo za kiserikali, sekta binafsi, vyombo vya habari, na wadau wa maendeleo. Aidha, kiongozi hiki kitatumiwa na viongozi wa serikali za mitaa, ngazi ya kata, vijiji/mtaa, shule, kamati za shule, walimu, wazazi/walezi na jamii kwa ujumla.



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 12 15/04/2023 15:39

## SEHEMU YA PILI

## MAZINGIRA WEZESHI KATIKA MALEZI, MAKUZI NA MAENDELEO YA AWALI YA MTOTO

### 2.1 Utangulizi

Malezi, ya awali ya mtoto ni huduma anayoipata mtoto ili kukidhi mahitaji yake kimwili, kiakili, kijamii na kihisia kuanzia miaka 0 - 8. Huduma hizi hujumuisha lishe bora, malazi bora, ulinzi na usalama wa mtoto, ushauri na unasihi, matendo changamshi, na afua stahiki kwa watoto wenye mahitaji maalumu. Vitendo changamshi hufanyika kupitia katika michezo, nyimbo, hadithi, majigambo, ushauri na faraja katika kukuza lugha kwa mtoto, pamoja na ukuzaji wa stadi za awali za kusoma, kuandika na kuhesabu. Mazingira wezeshi ni muhimu ili kujenga utayari wa kujifunza. Mazingira wezeshi hujumuisha mazingira ya utendaji na mazingira ya kisaikolojia kwa pamoja hukuza utayari wa kucheza, kujifunza na kupata maendeleo kiakili, kimwili, kijamii, na kihisia.

Mazingira wezeshi hukuza ari ya mtoto kuendelea kujifunza na kuibua stadi mbalimbali, zikiwamo stadi za awali za kusoma, kuandika na kuhesabu.



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 13 15/04/2023 15:39

Upatikanaji wa huduma na afua stahiki kwa pamoja huendeleza makuzi na ujifunzaji kwa ajili ya maendeleo ya jumla ya mtoto kupitia katika hatua muhimu tofauti za ukuaji na ujifunzaji. Hatua za ukuaji huenda sambamba na uchangamshi wa awali wa mtoto kama inavyoelezwa kwa ufupi katika Jedwali Na 1.

**Jedwali Na. 1: Hatua za Ukuaji na Uchangamshi wa Awali wa Mtoto**

| Umri | Matendo Kulingana na Hatua za Makuzi | Matendo Changamshi |
|---|---|---|
| **Miezi 0 - 6** | Kulia<br>Kutembeza macho<br>Kugeuza shingo<br>Kutofautisha sauti<br>Kutabasamu na Kucheka<br>Kuitikia<br>Kustuka akisikia kelele<br>Kugugumia<br>Kutoa ukulele sauti<br>Kubwabwaja/ kububujika<br>Kuchezea mate | Kumpatia vifaa vya michezo ning'inizi, vinavyong'aa na vyenye kutoa milio mbalimbali<br>Kumbembeleza, kumwimbia na kuzungumza nae<br>Kumwonyesha upendo na ukaribu<br>Kuongea na kucheza naye kwa tabasamu<br>Kuongea naye<br>Kufuatilia maendeleo yake hatua kwa hatua |



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 14 15/04/2023 15:39

| Umri | Matendo Kulingana na Hatua za Makuzi | Matendo Changamshi |
|---|---|---|
| **Miezi 7 - 12** | Kutamka neno mojamoja<br>Kusemasema yasiyoeleweka<br>Kucheza michezo mbalimbali<br>Kuimba kwa kurudiarudia<br>Kutofautisha na kufananisha rangi<br>Kufuatisha maneno ya wengine | Kupewa mazoezi rahisi ya mwili<br>Kupewa vitu vyenye kutoa sauti na milio mbalimbali<br>Kupewa vifaa vya michezo vyenye rangi za msingi<br>Kupewa upendo na ukaribu<br>Kuzungumza naye<br>Kutomtenga na watoto wengine<br>Kufuatilia maendeleo yake hatua kwa hatua |
| **Mwaka 1 - 2** | Kupanga na kupangua vitu<br>Kutofautisha<br>Kushika viandikia<br>Kujieleza kwa kurudirudia<br>Kutamka maneno na namba | Kupewa mazoezi rahisi ya mwili na vitendo vya ujifunzaji<br>Kupewa vitabu vya picha rahisi<br>Kupewa vifaa vya michezo vyenye rangi za msingi |



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 15 15/04/2023 15:39

| Umri | Matendo Kulingana na Hatua za Makuzi | Matendo Changamshi |
|---|---|---|
| | Kuimba nyimbo rahisi<br>Kuuliza maswali rahisi<br>Kuitikia ndiyo na hapana<br>Kuandikaandika<br>Kuchora na kusiriba<br>Kuchapa maumbo ya vitu anavyoviona | Kupewa upendo na ukaribu<br>Kutumia sentensi za maneno mawili<br>Kufuatilia maendeleo yake hatua kwa hatua<br>Kutumia michezo kupima matokeo ya ujifunzaji |
| **Miaka 3 - 4** | Kuongeza msamiati<br>Kuonyesha upendo<br>Kudhibiti hisia<br>Kujieleza<br>Kutamka namba<br>Kuhusianisha namba na vitu<br>Kusoma herufi msingi<br>Kutamka sentensi fupi | Kupewa mazoezi ya kutosha na vitendo vya ujifunzaji<br>Kupewa vitabu vya picha rahisi<br>Kupewa vifaa vya michezo<br>Kupewa upendo na ukaribu<br>Kusimuliwa hadithi<br>Kuelekezwa namna ya kushika viandikia<br>Kupewa vifaa vya michezo |



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 16 15/04/2023 15:39

| Umri | Matendo Kulingana na Hatua za Makuzi | Matendo Changamshi |
|---|---|---|
| | | Kufuatilia maendeleo yake hatua kwa hatua<br>Kutumia michezo kupima matokeo ya ujifunzaji |
| **Miaka 5 - 6** | Kujieleza kwa ufasaha<br>Kusimulia hadithi<br>Kucheza michezo na marafiki<br>Kuuliza maswali mengi<br>Kuhesabu na kusoma namba | Kupewa mazoezi ya kutosha na vitendo vya ujifunzaji<br>Kupewa vitabu rahisi vya kusoma na kuhesabu<br>Kupewa vifaa vya michezo<br>Kupewa upendo na ukaribu<br>Kufuatilia maendeleo yake hatua kwa hatua<br>Kutumia michezo kupima matokeo ya ujifunzaji |



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 17 15/04/2023 15:39

| Umri | Matendo Kulingana na Hatua za Makuzi | Matendo Changamshi |
|---|---|---|
| **Miaka 7 - 8** | Kujiamini<br>Kueleza hisia zake<br>Kusoma na kuandika<br>Kuongeza na kupunguza namba kwa ufasaha<br>Kusimulia matukio<br>Kucheza michezo inayojenga stadi | Kupewa mazoezi ya kutosha na masomo<br>Kupewa vitabu vya kusoma na kuhesabu<br>Kupewa vifaa vya michezo<br>Kupewa upendo na ukaribu<br>Kufuatilia maendeleo yake hatua kwa hatua<br>Kutumia michezo kupima matokeo ya ujifunzaji |

Rejea Kitabu cha Malezi na Ujifunzaji Hatua ya I, 2019

## 2.2 Uwekezaji katika Mazingira ya Ujifunzaji

Uwekezaji katika mazingira ya ujifunzaji ni muhimu katika kujenga utayari wa mtoto kujifunza kwa ufanisi. Mazingira wezeshi yanahusisha shule/darasa lenye mazingira rafiki yanayochochea utayari wa mtoto kujifunza kikamilifu. Mazingira haya ni pamoja na mazingira ya utendaji ya ndani na nje kumwezesha mtoto kujenga utayari wa kujifunza. Mambo ya kuzingatia ni:



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 18 15/04/2023 15:39

i. Michezo ya utendaji kukuza mawasiliano, ubunifu na fikra tunduizi;
ii. Kutumia zana zinazomshirikisha mtoto zinazopatikana kwenye mazingira husika;
iii. Ushirikiano kati ya mwalimu wa darasa la kwanza na mwalimu wa Elimu ya Awali;
iv. Kuandaa miundombinu rafiki kwa kuzingatia mahitaji ya kila mtoto;
v. Kuwa mnyumbufu na mbunifu kwa kuzingatia muktadha wa ujifunzaji; na
vi. Kufuatilia maendeleo ya mtoto hatua kwa hatua.

### 2.2.1 Michezo na Maendeleo ya Mtoto

Michezo huhusisha vitendo huru vilivyochaguliwa na kufanywa na watoto kutokana na ubunifu na msukumo wa ndani katika uchaguzi na uchezaji.

Watoto huchangamana na kuelewana wanapocheza pamoja. Watoto wanajifunza mengi kutokana na michezo kwa kuwa inawafundisha stadi za maisha, kuwasiliana, kushirikishana, kukubaliana, kuwa na nidhamu na uvumilivu kwa wenzao. Kuna aina tofauti za michezo ya utendaji ambayo hujumuisha michezo ya ushindani, nyimbo, hadithi, majigambo ya watoto, michezo ya kuigiza na michezo inayofuata taratibu.



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 19 15/04/2023 15:39

Umuhimu wa michezo kwa maendeleo ya mtoto hauna mipaka. Kupitia michezo mtoto huweza kuimarika katika njia zifuatazo: uratibu wa mfumo wa mwili na mjongeo, stadi za misuli midogo na misuli mikubwa, fursa za makuzi ya ubongo na imani, stadi za lugha na mawasiliano, mabadiliko ya kawaida ya hisia na uzoefu, kufikiri na ubunifu, vinavyomuwezesha kufanikiwa katika maisha yake ya baadaye. Kupitia mchezo watoto hujifunza kuthubutu, kufurahi, upendo, kushiriki kikamilifu katika mijadala kama sehemu ya ujifunzaji. Stadi hizi humwezesha mtoto kukua na kuwa na mafanikio yake, familia, jamii, na taifa.

### 2.2.2 Kuzingatia Kanuni Zinazoongoza Malezi na Uchangamshi wa Awali wa Mtoto

Katika kutoa huduma stahiki kwa ajili ya maendeleo ya jumla ya watoto, wadau wa Elimu ya Awali, wakiwamo wazazi/walezi wanatakiwa kuzingatia kanuni zifuatazo:

i. **Maslahi mapana ya mtoto:** kufanya kazi wakitanguliza maslahi mapana ya watoto wanaowahudumia katika muktadha wa ulinzi, kuhimiza, na kutekeleza haki zao. Pamoja na hayo, mahitaji yote ya makuzi



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 20 15/04/2023 15:39

ya mtoto na ujifunzaji wa awali yanatakiwa kuendelezwa.

ii. **Usiri na ufaragha:** kuhakikisha kuwa taarifa za mtoto na famili zinatunzwa kwa usiri.

iii. **Ushirikeli:** kuelewa hisia za watoto na kuzifanyia kazi.

iv. **Kutobagua:** Huduma za malezi makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto zinatakiwa kuwafikia watoto wote bila kujali jinsi, eneo, dini au ulemavu.

v. **Maendeleo jumui:** Makuzi ya watoto ni jumui. Hivyo, maeneo yote ya kijamii, kihisia, kifikra, na kimwili yanatakiwa kupewa uzito sawa.

vi. **Kushiriki na kushirikishwa:** kuelewa kuwa watoto na familia zao wana haki ya kushiriki na kushirikishwa kikamilifu katika masuala yote yanayowahusu.

vii. **Kuwajibika:** kutoa huduma za malezi, makuzi, na maendeleo ya awali ya mtoto zilizo sahihi na bora na zenye manufaa kwa watoto wote bila ubaguzi

viii. **Tamaduni zinazofaa:** kuzingatia mila na desturi zinazokubalika na ambazo hazina madhara kwa watoto kwa muktadha wa



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 21 15/04/2023 15:39

eneo wanaloishi, mazingira ya ujifunzaji, na miiko ya kijamii.

ix. **Usafi, usalama na mpangilio:** kuelewa kuwa mtoto anahitaji kukua na kulelewa katika mazingira ambayo ni safi na salama. Mtoto aelekezwe kuzingatia usafi, usalama na mpangilio wa vitu anavyovitumia katika michezo na maisha yake kwa ujumla.

### 2.2.3 Mazingira ya Ndani ya Darasa

Mazingira ya ndani ya darasa yanapaswa kujumuisha masuala muhimu yafuatayo:

i. Umahiri wa mwalimu kuandaa mazingira wezeshi kwa kuzingatia mitindo ya ujifunzaji wa mtoto na kujenga utayari wa kujifunza kulingana na vionjo vyake. Aidha, mwalimu na watoa huduma wengine wanapaswa kuchangamana vizuri na watoto ili kujenga hamasa ya ujifunzaji kwa kila mtoto. Vilevile, mwalimu na watoa huduma wengine wanatakiwa waweke utaratibu wa kupima maarifa ya awali aliyonayo mtoto. Endapo itabainika kuwa mtoto ana changamoto za ujifunzaji, afua stahiki itahitajika ili kurekebisha changamoto hizo;

ii. Shughuli za kutendwa na mtoto



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 22 15/04/2023 15:39

zimeandaliwa kwa kuzingatia umri, mahitaji ya kila mtoto na kwa kuhamasisha matumizi ya milango ya fahamu kumjenga mtoto kiakili, kimwili, kijamii, na kihisia;

iii. Matumizi ya zana za ujifunzaji na ufundishaji zenye uwiano sawa na idadi ya watoto darasani, zinazovutia, rafiki, jumuishi, zinazochochea ujifunzaji, zilizoning'inizwa, na kupangiliwa ili zifikiwe kirahisi na watoto. Aidha, zana zilizobandikwa ukutani, ziwekwe kulingana na upeo wa macho ya watoto.

    Vilevile, zana zipatikane kutokana na mazingira halisi na zisiwe za gharama kubwa;

iv. Matumizi stahiki ya Muhtasari na machapisho mengine ambayo ni mwongozo wa mwalimu wa kufundishia Elimu ya Awali, vitabu vya kiada na ziada, vitabu vya hadithi na rejea za malezi, makuzi na maendeleo ya mtoto;

v. Matumizi stahiki ya kona za ujifunzaji, zikiwamo kona za lazima kwa mujibu wa Mtaala wa Elimu ya Awali: kona ya hisabati, kona ya michezo na kona ya lugha (kusoma



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 23 15/04/2023 15:39

na kuandika). Kona nyingine za ujifunzaji zinaweza kuongezeka kulingana na nafasi ya chumba cha darasa, idadi ya watoto na mahitaji yao. Aidha, kila kona inatakiwa iwe na zana zinazojenga utayari wa mtoto kwa kuwa na maudhui yanayorejelea muktadha wa ujifunzaji. Zana zinazowekwa katika kila kona ziwe safi na salama na zitunzwe kwenye kifaa ambacho kina jina la zana husika; na

vi. Matumizi stahiki ya chumba cha darasa chenye sifa stahiki kulingana na miongozo na mahitaji ya mtoto: usafi, usalama, mpangilio, na hewa ya kutosha. Aidha, chumba kiwe na zana za kutosha za ujifunzaji kuwawezesha watoto kuwa tayari na kushiriki kikamilifu katika ujifunzaji.

### 2.2.4 Mazingira ya Nje ya Darasa

Mazingira ya nje ya darasa yanahusisha:

i. Matumizi stahiki ya eneo la mchanga na maji linalozingatia kujenga dhana ya vipimo: stadi ya ulinganifu, kuzama na kuelea, uzito na wepesi, na kijifunza wingi na uchache, pamoja na kuumba na kuunda;

ii. Matumizi stahiki ya michezo ya utendaji



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 24 15/04/2023 15:39

wa mwili na vifaa vyake ili kuwawezesha watoto kuwa tayari kucheza na kujifunza. Michezo hiyo inaweza kuwa ya mtoto mmojammoja, michezo ya jozi pamoja na michezo ya vikundi. Michezo ilenge misuli midogo na mikubwa, utendaji wa macho na mikono, mijongeo ya mwili na wepesi wa kutenda.

iii. Michezo ya utendaji ni pamoja na kubembea, kuruka na kupita katikati ya matairi, kuvuta kamba, kucheza mpira, kubembea, kuteleza, na kukimbia kufuata mitindo ya uchezaji (kukimbia kinyumenyume kwa mguu mmoja, kwa magunia, kukimbiza kuku, na mbio za kupokezana vijiti); na

iv. Kutumia mazingira safi na salama kujifunza: kuchunguza vitu, matendo ya watu, wadudu na wanyama. Kuwaelekeza watoto kuweka tahadhari kuepuka majanga yanayoweza kusababishwa na moto, maji, mashimo hatarishi barabara, vichaka, visima, na vilabu vya pombe.

### 2.2.5 Mafunzo Endelevu kwa Walimu Kazini

Uwekezaji katika taaluma na utaalamu kwa mwalimu wa Elimu ya Awali ni muhimu katika



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 25 15/04/2023 15:39

kuboresha utoaji wa Elimu ya Awali. Mpango wa mafunzo kazini huandaliwa ili kuwaendeleza walimu kitaaluma na kiutaalamu wakiwa kazini kwa njia ya ana kwa ana, na ya masafa ili wasiathiri vipindi vya masomo. Ni vema mafunzo haya yakalenga kuwaendeleza walimu kazini ili kutatua changamoto za ujifunzaji pamoja na kuwawezeshe watoto kujifunza kikamilifu.

#### 2.2.5.1 Uandaaji wa Mafunzo ya Walimu Kazini

Mafunzo ya walimu kazini huandaliwa panapokuwa na mahitaji ya walimu kujengewa uwezo wa kumudu ufundishaji na ujifunzaji wenye ufanisi ili kukidhi mahitaji ya mtoto wa Elimu ya Awali. Ili kuandaa mafunzo haya ni vyema kuzingatia mambo yafuatayo:

i. Kubainisha mahitaji ya walimu kitaaluma na kitaalamu;

ii. Kubaini hali halisi ya utekelezaji wa mtaala wa Elimu ya Awali pamoja na changamoto za watoto kushindwa kumudu stadi za awali za kusoma, kuandika na kuhesabu;

iii. Kubaini umahiri alionao mwalimu katika kuandaa mazingira ya ujifunzaji na namna ya kukabiliana na changamoto za ujifunzaji wa mtoto;

iv. Kuandaa mpango wa muda mfupi na wa muda mrefu wa mafunzo ya walimu kazini;
v. Kupata maoni ya wazazi/walezi, jamii na wadau wengine kuhusiana na maendeleo ya watoto kitaaluma;
vi. Kuweka utaratibu wa kushiriki mafunzo bila kuathiri ujifunzaji wa watoto darasani;
vii. Kuimarisha mawasiliano miongoni mwa walimu ili kuinuana kitaalauma na kiutaalamu; na
viii. Kuweka utaratibu wa walimu kujitathmini wenyewe na kubaini changamoto za ufundishaji na ujifunzaji (fomu ya tathmini binafsi ya mwalimu).

Mafunzo ya walimu kazini yanaweza kuwa ya muda mfupi au mrefu kutegemea na mahitaji ya ujifunzaji pamoja na aina ya mafunzo yanayotakiwa kutolewa. Njia za utoaji wa mafunzo katika Elimu ya Awali kama zilivyobainishwa katika Kiunzi cha Taifa cha Mafunzo Endelevu ya Walimu: Elimu masafa, mafunzo ya ana kwa ana katika klasta/Kituo cha walimu, warsha na makongamano ya kitaaluma na kitaalamu na kupitia tovuti za ujifunzaji. Mfumo tofauti wa utoaji wa mafunzo kazini kwa walimu wa Elimu ya Awali:

i. Mafunzo ngazi ya shule/kituo cha kazi;
ii. Mafunzo ngazi ya kata; na



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 27 15/04/2023 15:39

iii. Mafunzo ya kitaaluma kwa walimu kazini kwenye taasisi zinazotambulika.

#### 2.2.5.2 Jinsi ya Kubaini Mahitaji ya Walimu kwa Ajili ya Mafunzo Endelevu Kazini

Mafunzo endelevu ya walimu kazini huandaliwa baada ya kubainisha mahitaji ya walimu kutokana na taarifa za tathmini binafsi ya walimu wa Elimu ya Awali (angalia fomu) ya tathmini binafsi ya mwalimu, tathmini ya wathibiti ubora, pamoja na tathmini binafsi ya shule). Kabla ya Mafunzo ni vyema walimu wajaze fomu ya kujitathimini ili kubaini kiwango chao cha taaluma na utaalamu na kweza kutoa mafunzo ya kuboresha utendaji wao. Umuhimu wa kufanya tathmini hii ni:

i. Kubaini maeneo ya kuwekea msisitizo wakati wa mafunzo;
ii. Kuandaa programu ya mafunzo endelevu kazini kukidhi mahitaji ya walimu;
iii. Kujenga uwezo kwa walimu kuongeza ubora katika utendaji wao; na
iv. Kupima matokeo ya ujifunzaji na kutunza kumbukumbu sahihi.

Mafunzo endelevu ya walimu kazini yanatakiwa kuandaliwa kwa kuzingatia mahitaji ya walimu, changamoto



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 28 15/04/2023 15:39

zinazowakabili walimu pamoja na mabadiliko ya sayansi na teknolojia ili kuwezesha mambo yafuatayo:

i. Kushirikisha walimu katika uandaaji na uendeshaji wa mafunzo ili kuinua kiwango cha taaluma na utaalamu wa mwalimu;

ii. Ubora wa mafunzo yatolewayo kuzingatia mtaala na vifaa vyake;

iii. Kuwezesha ubunifu na unyumbufu wa mwalimu wa Elimu ya Awali kuandaa mazingira wezeshi ya ujifunzaji wa watoto, wakiwamo wenye mahitaji maalumu;

iv. Ushirikishwaji wa jamii kufanikisha utoaji wa mafunzo endelevu kazini; na

v. Kutoathiri ratiba ya ufundishaji wa mwalimu shuleni.

#### 2.2.5.3 Ushirikishaji wa Wadau wa Elimu katika Utoaji Mafunzo

Uendeshaji wa mafunzo endelevu kazini unatakiwa kuwa shirikishi ili kujenga dhana ya uendelevu. Baadhi ya wadau wanaopaswa kushirikishwa ni:

i. Walimu wanaohitaji mafunzo;

ii. Jamii;

iii. Maafisa Elimu Kata, Wilaya na Mkoa;



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 29 15/04/2023 15:39

iv. Wathibiti Ubora wa Shule;

v. Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa;

vi. Taasisi na mashirika mbalimbali yanayojihusisha na utoaji wa elimu; na

vii. Asasi za kiraia na mashirika ya kimataifa yanayotoa mafunzo katika elimu.

#### 2.2.5.4 Umahiri Unaotakiwa Kujengwa

Mafunzo yatolewe kwa kuzingatia maeneo ya umahiri yafuatayo:

i. Malezi, makuzi na maendeleo ya mtoto;

ii. Ukuaji wa lugha kwa mtoto;

iii. Stadi za awali za kusoma, kuandika, na kuhesabu;

iv. Utambuzi wa mapema wa watoto wenye mahitaji maalumu na utoaji wa afua stahiki;

v. Malezi na unasihi;

vi. Stadi za maisha;

vii. Ujifunzaji kwa michezo na upimaji wa matokeo ya ujifunzaji;

viii. Uongozi na utawala wa darasa; na

ix. Kumudu darasa changamani.



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 30 15/04/2023 15:39

### 2.2.6 Ushiriki wa Familia na Jamii katika Kutoa Huduma Stahiki

Mambo ya kuzingatia wakati wa kushirikisha jamii katika kutoa huduma stahiki kwa maendeleo ya mtoto ni pamoja na:

i. Kumshirikisha mtoto katika shughuli za kifamilia zinazojenga uwezo wa kukabiliana na changamoto katika mazingira yake;
ii. Kushiriki michezo pamoja na mtoto akiwa nyumbani;
iii. Kuwawezesha watoto kusimulia hadithi na visa mafunzo vitakavyomjengea mtoto uwezo wa kusikiliza, kuzungumza na kutenda ipasavyo;
iv. Kumjengea mtoto uwezo wa kuhimili maono, kuwa na nidhamu ya kuwa mtiifu na kufuata maelekezo; na
v. Kutenda matendo yatakayomjengea mtoto uwezo wa kujiamini na kushirikiana na wenzake.

Ushirikishwaji wa wadau wengine wa elimu katika utekelezaji wa Elimu ya Awali ni muhimu sana ili ujifunzaji na ufundishaji uweze kutokea. Wadau hawa ni pamoja na:



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 31 15/04/2023 15:39

i. **Wizara na taasisi zake:** wizara na taasisi zake ziratibu, zihamasishe, na kusimamia utekelezaji fanisi wa Mtaala wa Elimu ya Awali ili kupata matokeo tarajiwa;

ii. **Mashirika yasiyokuwa ya kiserikali:** mashirika ya kiraia, taasisi za kidini, na mashirika ya kijamii yahamasishe utoaji wa huduma stahiki kuisaidia Serikali kufikia malengo yaliyowekwa katika utekelezaji wa Elimu ya Awali; na

iii. **Mashirika ya kimataifa:** mashirika haya yashirikiane na Serikali kuboresha mazingira ya ujifunzaji wa mtoto ili kufikia malengo yaliyowekwa katika Elimu ya Awali.

### 2.2.7 Kujenga Utayari na Ushiriki wa Mtoto

Utayari wa mtoto katika kujifunza humwezesha mtoto kushiriki kikamilifu katika kutenda ipasavyo. Mtoto anapotenda anajifunza dhana mbalimbali kutokana na mazingira yanayomzunguka na kujenga maana. Utayari wa mtoto kujifunza unahusisha utayari wa kimwili, kiakili, kiroho na kiuhusiano.

#### 2.2.7.1 Utayari wa Mtoto Kimwili

Mwezeshe mtoto kufanya matendo changamshi yanayojenga utayari wa kimwili ili kuwezesha:

i. Mijongeo ya mwili;



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 32 15/04/2023 15:39

ii. Utimamu wa viungo vya mwili katika utendaji;
iii. Kusikiliza, kuzungumza, kusoma, na kuandika;
iv. Kuruka na kutengeneza msawazo wa mwili;
v. Uratibu wa macho na mikono; na
vi. Kukuza misuli midogo na mikubwa.

### 2.2.7.2 Utayari Kiakili

Mwezeshe mtoto kufanya matendo changamshi yanayojenga utayari wa kiakili ili kumwezesha:

i. Kujenga kumbukumbu kwa kurudiarudia matendo;
ii. Kutoa mwitikio chanya, kujenga, na kupenda kutenda zaidi;
iii. Kufikiri, kudadisi na kutafakari;
iv. Kutatua matatizo na kupata ukweli;
v. Kuwa makini katika utendaji;
vi. Kujenga fikra tunduizi;
vii. Kufanya vitu kwa mpangilio sahihi; na
viii. Kuhusianisha na kutofautisha vitu katika mazingira.



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 33 15/04/2023 15:39

#### 2.2.7.3 Utayari Kiroho na Kimaono

Mwezeshe mtoto kufanya matendo changamshi yanayojenga utayari wa kiroho na kimaono ili kumwezesha kufanya vitendo vyenye mwelekeo chanya vinavyomwezesha mtoto:

i. Kukubali kutenda kwa moyo wote;
ii. Kushiriki kutenda pamoja na wenzake;
iii. Kujijali na kuwajali wengine;
iv. Kuthamini utu na vitu;
v. Kutii sheria na taratibu zilizopo;
vi. Kuwa na hofu ya Mungu; na
vii. Kujitambua na kujikubali.

#### 2.2.7.4 Utayari wa Mtoto Kisaikolojia

Mwezeshe mtoto kufanya matendo changamshi yanayojenga utayari wa mtoto kisaikolojia ambapo itamwezesha kupima au kuchunguza tabia, miitikio na mienendo. Matokeo ya uchunguzi hutoa taarifa ambazo husaidia kuwaelewa watoto na kuwaongoza kufuata njia sahihi za malezi ili waweze kukubalika katika jamii. Ili kumjenga mtoto kisaikolojia, ni lazima kuzingatia yafuatayo:

i. Kubaini vyanzo vya tabia mbalimbali za watoto na kuelewa athari za tabia hizo;

ii. Kuchunguza matendo ya watoto na kuelewa tofauti za tabia zao kulingana na mahitaji yao ili kutoa afua stahiki za kurekebisha tabia zisizofaa;
iii. Kujenga mtazamo chanya wa kumudu tabia njema kwa kuonya dhidi ya tabia mbaya, kudhibiti tabia mbaya zilizoanza kujitokeza na kuendeleza tabia inayokubalika;
iv. Kutoa fursa kwa mtoto kushiriki katika matendo changamshi ya ujifunzaji kwa vitendo; na
v. Kufanya ufuatiliaji wa maendeleo ya mtoto mara kwa mara ili kubaini matokeo ya ujifunzaji.

#### 2.2.7.5 Utayari wa Mtoto Kijamii na Kiuhusiano

Mwezeshe mtoto kufanya vitendo changamshi vinavyojenga utayari wa mtoto kijamii na kiuhusiano ili kumwezesha kujenga uhusiano chanya, kutimiza wajibu, na kushirikiana na wengine katika kujifunza. Katika kumwandaa mtoto kijamii na kiuhusiano, mambo yafuatayo ni lazima yazingatiwe:

i. Matendo changamshi yanayomjenga mtoto kihaiba na kimwelekeo chanya katika kuheshimu utu, mila, na tamaduni za jamii



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 35 15/04/2023 15:39

husika;

ii. Kulinda haki za mtoto kwa kuzingatia sera, sheria, na taratibu zilizowekwa;

iii. Kuwawezesha watoto kushirikiana katika shughuli mbalimbali zinazokubalika;

iv. Kuweka na kutekeleza taratibu na kanuni zinazosimamia tabia na maadili ya watoto;

v. Kubaini watoto wenye mahitaji maalumu na kutoa afua stahiki;

vi. Kutoa fursa sawa kwa watoto kwa kuzingatia usawa wa kijinsia;

vii. Kujenga stadi za kujitambua, kujijali na kuwajali wengine, kujithamini na kuwathamini wengine, kujiheshimu na kuwaheshimu wengine;

viii. Kutumia mbinu na zana stahiki zinazochochea uhusiano na mawasiliano kwa watoto ili wasaidiane wao wenyewe; na

ix. Kuwawezesha watoto kushiriki pamoja matendo ya ubunifu na ya kuwasaidia kutawala hisia, kutatua matatizo yao wenyewe na kujenga stadi za maisha.



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 36 15/04/2023 15:39

### 2.2.8 Afua Stahiki kwa Mtoto Aliyefanyiwa Vitendo vya Ukatili

Jitihada za kuzuia vitendo vya ukatili kabla havijatokea zinatakiwa kuwekwa. Iwapo ukatili utafanyika kwa mtoto, ni lazima wazazi/walezi, walimu, na watoa huduma wengine kuelewa dalili za awali zinazoweza kumaanisha kuwa mtoto anafanyiwa vitendo hivyo. Aidha, unapogundua kuwa tatizo limetokea, unapaswa kufanya tathmini/uchunguzi wa awali ili kuweza kutoa afua stahiki.

Baadhi ya dalili zinazoonesha kuwa mtoto anafanyiwa au yuko kwenye hatari ya kufanyiwa vitendo vya ukatili na unyanyasaji ni pamoja na;

i. Mtoto kuwa na makovu yasioeleweka yanayoweza kuashiria kupigwa na kitu chenye ncha kali, kuungua, kung'atwa, kuvunjika n.k;

ii. Mtoto kushindwa kukaa au kutembea vizuri;

iii. Mtoto kupoteza kujiamini;

iv. Tabia za mtoto kubadilika ghafla, Mfano mtoto kuwa na hofu/kuwa mkimya/au kuongea kupita kiasi;

v. Mtoto kuwa na uelewa mkubwa wa mambo ya ngono;



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 37 15/04/2023 15:39

vi. Mtoto kujikojolea;

vii. Mtoto kuwa na hasira za kupitiliza;

viii. Mtoto kupoteza hamu ya kujifunza,

ix. Mtoto kujitenga; na

x. Mtoto kupoteza hamu ya kula au kula kupita kiasi cha kawaida.

***Angalizo:*** *Mlezi akumbuke kuwa hizi ni baadhi tu ya dalili ni muhimu sana ziangaliwe pamoja na umri, hatua ya ukuaji na maendeleo ya mtoto na ukomavu.*

## 2.3 Upatikanaji wa Huduma Stahiki

Upatikanaji wa huduma stahiki kwa watoto unasaidia kuweka mazingira wezeshi ya utoaji wa Elimu ya Awali. Huduma stahiki zinazopaswa kupatikana zimefafanuliwa katika vipengele vinavyofuata.

### 2.3.1 Huduma ya Afya

Mwezeshe mtoto kuwa na afya ya mwili ambayo ni muhimu kwa ustawi wake, hususan: katika makuzi na maendeleo yake katika nyanja zote, yaani kiakili, kimwili, kijamii na kimaono. Katika kuhakikisha kuwa afya ya mtoto inakuwa nzuri, ni lazima kuzingatia mambo yafuatayo:

i. Kuweka utaratibu wa kumpima mtoto vipimo vya urefu na uzito ili kubaini makuzi



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 38 15/04/2023 15:39

na maendeleo yake kimwili;

ii. Kufuatilia taarifa za maendeleo ya mtoto kiafya katika kituo cha afya au zahanati iliyo karibu na shule kwa kushirikisha wazazi/walezi ili kubaini mtoto mwenye matatizo ya kiafya na kutoa afua stahiki;

iii. Kufanya uchunguzi wa kitabibu kwa walimu na watoa huduma wengine shuleni kila baada ya miezi sita ili kupata uthibitisho wa kutokuwa na magonjwa ya kuambukiza;

iv. Kuweka sanduku la huduma ya kwanza lenye vifaa na dawa muhimu na kuhifadhiwa sehemu salama mbali na watoto;

v. Vyoo vya watoto vizingatie watoto wenye mahitaji maalumu, umri, usafi, usalama pamoja na uwiano stahiki kulingana na miongozo;

vi. Kutunza kumbukumbu za afya za watoa huduma na huduma zilizotolewa; na

vii. Kuwe na chumba cha kupumzikia watoto chenye kitanda na godoro.

### 2.3.2 Utambuzi wa Awali na Utoaji wa Afua

Utambuzi wa awali hufanyika kwa mtoto ili kubaini mahitaji ya ujifunzaji, vipaji na vipawa



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 39 15/04/2023 15:39

vya mtoto pamoja na changamoto za ujifunzaji ili kutoa afua stahiki. Kuna namna mbalimbali za kuwatambua watoto kama inavyoelezwa katika sehemu zinazofuata:

i. Zingatia mahitaji ya mtoto kiakili, kimwili, kijamii, na kihisia;
ii. Mpime mtoto peke yake bila kufanya ulinganifu;
iii. Fuatilia vitendo vyake akiwa peke yake, katika jozi ama katika kundi bila kutumia mitihani na majaribio mengine;
iv. Fuatilia vitendo vyake na hatua ya makuzi yake kulingana na umri wake;
v. Bainisha viashiria vya makuzi yake kutokana na utendaji wake; na
vi. Onesha kiwango alichofikia ndipo utafute ufumbuzi wa tatizo.

### 2.3.3 Namna ya Kuwatambua Watoto Kutokana na Changamoto Walizonazo

Elimu ya Awali ni jumuishi inawalenga watoto wenye mahitaji tofauti ya ujifunzaji, wakiwamo wenye uoni hafifu, ualibino, ukiziwi, ukiziwi kutoona, ulemavu wa akili, usonji, vipawa na vipaji, changamoto za kiafya, changamoto za



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 40 15/04/2023 15:39

kihisia, changamoto za kitabia, changamoto za ujifunzaji, na ulemavu wa viungo,

### 2.3.3.1 Kumtambua Mtoto mwenye Changamoto za Uoni

Zingatia dalili zilizobainishwa kuweza kumtambua mtoto mwenye changamoto ya uoni ili kutafuta afua stahiki kama zilivyoelezwa katika Jedwali Na. 2.

**Jedwali Na. 2: Kumtambua Mtoto mwenye Changamoto za Uoni**

| Namna ya Kumtambua | Afua Stahiki kwa wenye Uoni Hafifu |
|---|---|
| • Jicho kuchezacheza kusiko kwa kawaida<br>• Mwonekano wa jicho usio wa kawaida kwa mfano jicho kuwa kubwa au dogo, kuwa na kovu au mtoto wa jicho<br>• Kusogea karibu sana na kitu ili aweze kukiona<br>• Kukaza sana macho wakati wa kusoma au kuangalia kitu, hasa chenye umbo dogo | • Maandishi yaliyokuzwa yatumike kwa wale watakaoweza kuyasoma baada ya upimaji<br>• Mtoto akae sehemu stahiki darasani<br>• Mtoto apewe viookuza endapo maandishi yaliyokuzwa hayakuandaliwa<br>• Kuwe na kiwango stahiki cha mwanga darasani |



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 41 15/04/2023 15:39

| Namna ya Kumtambua | Afua Stahiki kwa wenye Uoni Hafifu |
|---|---|
| • Kuona kwa shida katika sehemu yenye mwanga hafifu<br>• Kuacha baadhi ya herufi wakati wa kuandika ama kusoma<br>• Kupata tabu kutambua sura ya mtu/vitu hasa anapokuwa au vinapokuwa mbali<br>• Kujigonga mara kwa mara kwenye vitu wakati wa kutembea<br>• Malalamiko ya kichwa au macho kuuma mara kwa mara<br>• Kuona kwa tabu wakati wa usiku<br>• Kutumia fimbo nyeupe wakati wa kutembea<br>• Kuongozwa wakati wa kutembea<br>• Kutembea kwa woga na kujihami | • Mtoto apewe kibao henamu (reading/writing stand) ili kupunguza umbali kutoka chanzo cha kusoma na kuandika<br>• Mtoto apatiwe rufaa stahiki<br>• Kama uoni wa mtoto ni wa kumwezesha kufanya baadhi ya shughuli (functional vision), aelekezwe namna ya kutumia maandishi ya braille<br>• Kwa wasioona kabisa:<br>► Mzazi/mlezi ampeleke mtoto katika shule stahiki<br>► Mtoto aelekezwe jinsi ya kutumia vifaa vya braille<br>► Mwalimu atumie zana mguso za kufundishia na kujifunzia (tactual aids)<br>• Mtoto ajumuishwe na wenzake wakati wa ujifunzaji ili kuondoa hali ya kujitenga |



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 42 15/04/2023 15:39

| Namna ya Kumtambua | Afua Stahiki kwa wenye Uoni Hafifu |
|---|---|
| • Kutomudu mazingira ipasavyo<br>• Kutomaliza kwa wakati kazi anazopewa | • Mtoto apewe muda wa kutosha/ziada wa kufanya kazi anazopangiwa tofauti na ule wa ratiba ya kawaida |

Vifaa vinavyoweza kutumika kumtambua mtoto mwenye changamoto za uoni. Mtoto mwenye changamoto za uoni anaweza kutambuliwa kwa kutumia vifaa mbalimbali vikiwamo hivi vifuatavyo:

i. Futikamba;
ii. Vifaa vya kupimia uwanda wa uoni kama vile chati ya herufi;
iii. Vifaa vya kupimia kiwango cha mwanga na aina za rangi;
iv. Viookuza;
v. Tochi ndogo; na
vi. Kifaa tobwe.

### 2.3.3.2 Kumtambua Mtoto mwenye Ualbino

Mambo yanayoweza kusaidia kumtambua mtoto mwenye ualibino na afua stahiki kumsaidia mtoto husika ni kama yalivyobainishwa kwenye Jedwali Na. 3.



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 43 15/04/2023 15:39

**Jedwali Na. 3: Kumtambua Mtoto mwenye Changamoto za Ualibino**

| Namna ya Kumtambua | Afua Stahiki kwa Wenye Ualbino |
|---|---|
| • Kuwa na rangi ya ngozi, nywele au macho tofauti na asili yake<br>• Kufumba/kufinya macho kwenye mwanga mkali<br>• Macho kuchezacheza (nystigmus)<br>• Kutokuona au kuona kwa shida vitu vilivyo mbali<br>• Kuweka kichwa upande wakati wa kusoma au kuandika<br>• Macho kutoka machozi hasa kwenye mwanga mkali<br>• Kufikicha macho<br>• Vidonda kwenye ngozi hasa katika maeneo yaliyo wazi | • Awekwe katika eneo sahihi darasani kulingana na uoni wake<br>• Apatiwe miwani ya kupunguza mwanga wa jua<br>• Apewe viookuza ili vimsaidie kusoma na kuandika<br>• Apewe kibao henamu (reading /writing stand) ili kupunguza umbali wa macho na daftari/kitabu<br>• Apatiwe kofia na nguo za kufunika sehemu za wazi za mwili ili kumkinga dhidi ya miale ya mwanga wa jua<br>• Apewe mafuta ya kumsaidia kukinga ngozi dhidi ya miale ya jua<br>• Apewe vitabu vyenye maandishi yaliyokuzwa |



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 44 15/04/2023 15:39

### 2.3.3.3 Kumtambua Mtoto mwenye Ukiziwi

Ukiziwi ni hali ya kutokusikia kabisa au kusikia kwa shida na hali hiyo husababisha kushindwa au kutafsiri kwa shida lugha ya mazungumzo. Mambo yanayoweza kusaidia kumtambua mtoto mwenye ukiziwi na afua stahiki kumsaidia mtoto husika ni kama yalivyobainishwa kwenye Jedwali Na. 4.

**Jedwali Na. 4: Kumtambua Mtoto mwenye Ukiziwi**

| Namna ya Kumtambua | Afua Stahiki kwa wenye Ukiziwi |
|---|---|
| • Kushindwa kutoa sauti, kuchelewa kuongea au kujieleza<br>• Kuitika hata kama hajaitwa au kutoitika anapoitwa<br>• Kushindwa kufuata maelekezo ya mdomo na kurudiarudia sauti au maneno<br>• Kutokwa na usaha katika sikio moja au yote mawili | • Mwelekeze mtoto kufanya vitendo vinavyochochea uchangamshi wa awali kama vile kufungua na kufunga radio, kuchora na kupaka rangi<br>• Watoto wote wamwone mlezi/ mwalimu vizuri, na hasa uso na mdomo wake anapoongea<br>• Tumia zana zinazoonekana kama vile picha au vitu halisi wakati wa kutoa maelekezo ya ujifunzaji |



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 45 15/04/2023 15:39

| Namna ya Kumtambua | Afua Stahiki kwa wenye Ukiziwi |
|---|---|
| • Kuongea kwa sauti kubwa au ndogo<br>• Kushindwa kutofautisha sauti mbalimbali<br>• Kutembea kwa kuburuza miguu na kukosa msawazo wa mwili<br>• Kuangalia midomo ya mtu anayeongea<br>• Kutotambua chanzo na mwelekeo wa sauti<br>• Kutumia alama/ishara kuwasiliana<br>• Kuhitaji kurudiwarudiwa kwa neno au maneno | • Pasiwepo na sauti au kelele zozote zinazoingiliana na maelekezo<br>• Apatiwe shime sikio kulingana na kiwango chake cha baki ya usikivu<br>• Tumia lugha ya mawasiliano kamili (total communication) katika ujifunzaji<br>• Toa huduma za unasihi kwa wanafamilia ili wawe na uelewa wa kutosha juu ya watoto hao<br>• Jumuisha watoto ili waweze kuchangamana na kusaidiana katika ujifunzaji Vilevile, awepo mkalimani wa lugha ya alama pale inapobidi<br>• Mshirikishe mtoto kuandaa na kutumia kona ya ujifunzaji kujenga utayari wa kujifunza<br>• Toa ushauri wa rufaa inapobidi |



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 46 15/04/2023 15:39

Mtoto mwenye changamoto za ukiziwi anaweza kutambuliwa kwa kutumia vifaa mbalimbali. Jedwali Na. 5 linaonesha vifaa mbalimbali na jinsi ya kuvitumia ili kumbaini mtoto mwenye changamoto ya ukiziwi.

**Jedwali Na. 5: Vifaa na Matumizi katika Kumtambua Mtoto mwenye Ukiziwi**

| Jina la Kifaa | Matumizi |
|---|---|
| **Marimba** | Mshughulishe mtoto na michezo mbalimbali, kisha piga marimba au kitu kinachotoa sauti kuona kama mtoto atageuka kufuata sauti ilikotokea |
| **Manyanga** | Mzoeshe kuchezea manyanga |
| **Kengele ndogo** | Mzoeshe kupiga kengele |
| **Ngoma** | Mpigie ngoma karibu na sikio lake, kisha mpatie ngoma apige mwenyewe |
| **Filimbi** | Piga filimbi ukiwa kila upande wa sikio ili kuona mwitikio wake |
| **Vibonzo na Wanasesere** | Mwezeshe kutazama vibonzo na kusikiliza mwanasesere anayeongea akiguswa uone kama ataonesha ishara yoyote |



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 47 15/04/2023 15:39

Wakati wa kumtambua mtoto mwenye tatizo la ukiziwi, panahitajika watu wawili au zaidi. Mtu mmoja (mzazi/mlezi) anafanya kazi ya kumshughulisha mtoto na mtu mwingine (mwalimu/mpimaji/mtaalamu) ndiye anafanya kazi ya kugonga kitu kinachotoa sauti. Kwanza, kwa mbali na polepole, kisha anasogea karibu na kuongeza uzito au ukubwa wa sauti.

Mbali na kumtambua mtoto mwenye ukiziwi kwa kutumia vifaa vilivyotajwa katika Jedwali Na. 5, mwalimu atamtambua kwa kuangalia dalili/tabia zinazooneshwa katika kufanya upimaji kwa mtoto mwenye changamoto ya usikivu:

i. Hakikisha kuna mazingira tulivu na mwanga wa kutosha;
ii. Wakati unagonga kifaa chochote kinachotoa sauti, hakikisha mtoto haoni na wala kuhisi unachokifanya. Hii itakusaidia kupata matokeo halisi ya mwitikio wa mtoto;
iii. Gonga/puliza/bonyeza/piga kifaa kwa utaratibu maalumu kulingana na makusudi yalopangwa ili kitoe sauti;
iv. Wakati unagonga/unapiga/unapuliza au unabonyeza kifaa, mchunguze mtoto ili kubaini kama anasikia sauti; na
v. Weka kumbukumbu sahihi kwa kila hatua.



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 48 15/04/2023 15:39

#### 2.3.3.4 Kumtambua Mtoto mwenye Ukiziwi kutoona

Uziwi kutoona ni changamoto ya kukosa au kupungukiwa usikivu na uoni ambayo inaweza pia kuambatana na ulemavu wa akili na viungo. Hali hii inapojitokeza husababisha changamoto kubwa katika mfumo wa mawasiliano na ujongeaji. Tunaweza kumtambua mtoto mwenye ukiziwi kutoona kwa kuangalia dalili zinazooneshwa katika safu ya kushoto ya Jedwali Na.6.

**Jedwali Na 6: Kumtambua Mtoto mwenye Changamoto za Uziwi Kutoona**

| Namna ya Kumtambua | Afua Stahiki kwa wenye Ukiziwi kutoona |
|---|---|
| • Kutoongea<br>• Kutokujiamini wakati wa kutembea<br>• Kuitika hata kama hajaitwa au kutoitika anapoitwa<br>• Kutembea kwa kuburuza miguu na kukosa msawazo wa mwili | • Mtoto mwenye uoni hafifu amwone mlezi/mwalimu vizuri, hasa uso na mdomo wake anapoongea<br>• Pasiwepo na sauti au kelele zozote zinazoathiri ujifunzaji wa watoto |



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 49 15/04/2023 15:39

| Namna ya Kumtambua | Afua Stahiki kwa wenye Ukiziwi kutoona |
|---|---|
| • Kuongozwa wakati wa kutembea au kutumia fimbo nyeupe wakati wa kutembea<br>• Kuongea kwa sauti kubwa au ndogo<br>• Kuangalia midomo ya mtu anayeongea<br>• Kufikicha macho<br>• Malalamiko ya kichwa/ macho kuuma<br>• Kukosa mwitiko wa sauti<br>• Kutofuata maelekezo ya mdomo na kurudia sauti au maneno<br>• Kujitenga na wenzake<br>• Kutochangamka, kucheka au kushiriki michezo, hasa ya mzaha na utani<br>• Kuongeza sauti ya Radio/ TV<br>• Kukasirika haraka hasa bila sababu ya msingi | • Mwelekeze mtoto kufanya vitendo vinavyochochea uchangamshi, kwa mfano michezo mbalimbali kama kuogelea, kucheza mpira, na kutingisha mabega<br>• Wakati wa maelekezo ya ujifunzaji, tumia zana zinazoonekana, zana mguso, na zana za kusikiliza, picha, redio, na vitu halisi<br>• Apatiwe shime sikio kulingana na kiwango cha baki ya usikivu<br>• Kuwe na mwanga wa kutosha katika darasa la watoto wenye baki ya uoni<br>• Mtoto afundishwe namna ya kutumia lugha ya alama, lugha ya alama mguso na maandishi ya nukta nundu kulingana na mahitaji |



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 50 15/04/2023 15:39

| Namna ya Kumtambua | Afua Stahiki kwa wenye Ukiziwi kutoona |
| --- | --- |
| | • Wazazi/walezi na walimu wawapeleke watoto kwenye mazingira au maeneo stahiki ya ujifunzaji<br>• Toa huduma za unasihi kwa mtoto, walezi/wazazi na jamii inayowazunguka<br>• Toa ushauri wa rufaa<br>• Pasiwepo na sauti au kelele zozote zinazoingiliana na maelekezo |

Vifaa vilivyotajwa kwa ajili ya kusaidia katika kumtambua mtoto mwenye uziwi, vinaweza kutumika pamoja na vifaa vingine katika kumtambua mtoto mwenye uziwi kutoona kwa kufanya yafuatayo:

i. Onesha vitu mbalimbali vyenye rangi za kung'aa au hafifu pamoja na vitu vyenye maumbo tofauti ili kubaini uwezo wa mtoto kutofautisha rangi, ung'avu au uhafifu wa rangi pamoja na maumbo ya vitu;

ii. Gonga au gonganisha vifaa vinavyotoa sauti vilivyotajwa.



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 51 15/04/2023 15:39

### 2.3.3.5 Kumtambua Mtoto mwenye Ulemavu wa Akili

Ulemavu wa akili ni uwezo mdogo wa akili unaoambatana na utendaji wa chini ya wastani wa makuzi ya kawaida na kushindwa kumudu mazingira. Hali hii hujitokeza kuanzia miaka sifuri hadi kumi na minane (0 - 18). Mtoto mwenye ulemavu wa akili anaweza kutambuliwa kupitia dalili/tabia zilizooneshwa katika safu ya upande wa kushoto wa Jedwali Na. 7.

**Jedwali Na 7: Kumtambua Mtoto mwenye Ulemavu wa Akili**

| Namna ya Kumtambua | Afua Stahiki kwa wenye Ulemavu wa Akili |
|---|---|
| • Muonekano wa kimaumbile (Kichwa kikubwa/kidogo, sura ya mduara yenye macho madogo<br>• Kutokwa na udenda<br>• Kushindwa kuongea<br>• Utulivu au utundu kupita kiasi | • Kuchechemua/kusisimua milango ya fahamu<br>• Kuwashirikisha kwenye makundi wakati wa kujifunza<br>• Tumia zana na vitu halisi katika uelekezaji na ujifunzaji |



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 52 15/04/2023 15:39

| Namna ya Kumtambua | Afua Stahiki kwa wenye Ulemavu wa Akili |
|---|---|
| • Kushindwa kupambanua, kulinganisha na kupanga vitu kwa utaratibu<br>• Tabia zisizo za kawaida kama vile kucheka, kulia, na kununa bila sababu<br>• Kujisaidia bila utaratibu<br>• Kushindwa kutulia na kusikiliza kwa makini<br>• Kushindwa kujieleza (tatizo la mawasiliano) | • Mpatie vifaa stahiki vya kumjengea uwezo wa kufahamu mambo, kutofautisha vitu kwa ukubwa, rangi, umbile na kupanga kwa usahihi<br>• Mpongeze mtoto kwa kila hatua anayofanikiwa wakati wa ujifunzaji<br>• Tumia mbinu anuwai za ufundishaji na ujifunzaji<br>• Toa maelekezo machache na tumia vitendo zaidi<br>• Toa ushauri wa rufaa inapobidi |

Vifaa vinavyotumika kumtambua mtoto mwenye ulemavu wa akili ni hivi vifuatavyo:

i. Vibao jenga;

ii. Kadi mbalimbali (za maneno, picha, namba na michoro);

iii. Mipira ya rangi tofauti;



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 53 15/04/2023 15:39

iv. Shanga kubwa na ndogo za rangi mbalimbali;
v. Vibao fumbo;
vi. Sinia la namba;
vii. Midoli (mwanasesere);
viii. Kioo;
ix. Kamba;
x. Kalamu za risasi (penseli);
xi. Kalamu za rangi mbalimbali;
xii. Uzi;
xiii. Mkoba wa namba;
xiv. Vitabu mbalimbali;
xv. Karatasi; na
xvi. Sindano butu.

#### 2.3.3.6 Kumtambua Mtoto mwenye Usonji

Usonji ni athari iliyoko katika neva au milango ya fahamu ambayo hujitokeza kwenye ubongo na kuleta kasoro kubwa katika maeneo ya mawasiliano, uhusiano wa kijamii na utambuzi. Tunaweza kumtambua mtoto mwenye usonji kwa kuangalia dalili/ tabia zilizooneshwa katika safu ya upande wa kushoto wa Jedwali Na. 8.



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 54 15/04/2023 15:39

**Jedwali Na. 8: Kumtambua Mtoto mwenye Usonji**

| Namna ya Kumtambua | Afua Stahiki kwa wenye Usonji |
|---|---|
| • Kutotazamana uso kwa uso<br>• Kuchezea vitu vya hatari<br>• Kukosa woga<br>• Uharibifu wa vitu<br>• Kupenda kukaa peke yake (kujitenga)<br>• Kunguruma au kupiga kelele<br>• Kujidhuru au kudhuru watu wengine<br>• Kutembea kwa vidole vya miguu<br>• Kutabasamu nje ya muktadha<br>• Kujitingisha kwenda mbele na kurudi nyuma<br>• Kupenda kurudiarudia matendo<br>• Kutenda jambo moja kwa muda mrefu | • Kusisimua milango ya fahamu<br>• Kuwashirikisha kwenye makundi wakati wa kujifunza<br>• Tumia zana na vitu halisi katika uelekezaji na ujifunzaji<br>• Mpatie vifaa stahiki vya kumjengea uwezo wa kufahamu mambo, kutofautisha vitu kwa ukubwa, rangi, umbile na kupanga kwa usahihi<br>• Mpongeze mtoto kwa kila hatua anayofanikiwa wakati wa ujifunzaji<br>• Tumia mbinu anuwai za ufundishaji na ujifunzaji<br>• Toa maelekezo machache na tumia vitendo zaidi |



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 55 15/04/2023 15:39

| Namna ya Kumtambua | Afua Stahiki kwa wenye Usonji |
|---|---|
| | • Usimamizi wa karibu unatakiwa kuepuka kujidhuru<br>• Toa ushauri wa rufaa inapobidi |

**Kumtambua Mtoto mwenye Kipawa na/au Kipaji cha Kipekee**

Dhana ya vipawa na vipaji vya kipekee inafafanuliwa kuwa ni uwezo wa juu kiakili, kiubunifu na kiuongozi au ni uwezo wa kufanya vizuri katika nyanja maalumu za kitaaluma na sanaa. Mtoto mwenye kipawa na/au kipaji cha kipekee anaweza kutambuliwa kwa kuangalia dalili/tabia zilizoorodheshwa katika safu ya upande wa kushoto wa Jedwali Na. 9.

**Jedwali Na. 9. Kumtambua Mtoto Mwenye Kipaji na Kipawa**

| Namna ya Kumtambua | Namna ya Kutoa Afua Stahiki |
|---|---|
| • Hupenda kutoa msaada kwa wengine katika kujifunza | • Mpe mtoto kazi za kutosha, kulingana na uwezo na wepesi wake katika ujifunzaji |



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 56 15/04/2023 15:39

| Namna ya Kumtambua | Namna ya Kutoa Afua Stahiki |
|---|---|
| • Uwezo mkubwa wa kumbukumbu<br>• Tabia za kudakia na kuingilia jambo kabla ya wakati wake<br>• Wepesi wa kuelewa dhana mpya na msamiati wakati wa ujifunzaji<br>• Uwezo mkubwa wa kuongoza, kujieleza, kujiamini, kudadisi, kutatua na kubuni<br>• Hupenda kujifunza na kufanya kazi peke yake<br>• Umahiri na uwezo wa kukabiliana na changamoto<br>• Uwezo mkubwa wa kujifunza lugha mbalimbali<br>• Hufurahi sana wanapopewa kazi maalumu<br>• Kukosa utulivu kutokana na kazi zisizovutia au shughuli nyepesi kwake | • Mshirikishe katika ubunifu na ugunduzi katika kutatua matatizo ya ujifunzaji<br>• Uelewe ufahamu wake ili ukidhi mahitaji yake ya ujifunzaji<br>• Mpe fursa ya kuchangamana na watoto wenzake wasio na kipaji wala vipawa katika ujifunzaji<br>• Tumia mbinu na njia shirikishi, zana/vifaa na maandalizi ya kutosha kabla ya matendo ya ujifunzaji/ufundishaji<br>• Toa huduma za unasihi kwa mtoto wakati wa ujifunzaji |



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 57 15/04/2023 15:39

| Namna ya Kumtambua | Namna ya Kutoa Afua Stahiki |
|---|---|
| • Uwezo mkubwa katika stadi za kisanii | |

### 2.3.3.7 Kumtambua Mtoto mwenye Changamoto za Kiafya

Changamoto za kiafya ni hali ya mwili kutokuwa kawaida au kushindwa kufanya kazi yake ipasavyo. Hali hii husababishwa na kuwapo kwa magonjwa sugu kama vile pumu, VVU na UKIMWI, degedege, kifafa, kisukari, magonjwa ya moyo, selimundu, saratani, na malaria. Mtoto mwenye changamoto za kiafya anaweza kutambuliwa kwa kuangalia dalili zilizoorodheshwa katika safu ya upande wa kushoto wa Jedwali Na. 10.

**Jedwali Na. 10: Kumtambua Mtoto mwenye Changamoto za Kiafya**

| Namna ya Kumtambua | Namna ya Kutoa Afua Stahiki |
|---|---|
| • Kukonda kupita kiasi<br>• Kupoteza fahamu<br>• Kujiumauma | • Kufanya vitendo vinavyochochea uchangamshi wa awali |



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 58 15/04/2023 15:39

| Namna ya Kumtambua | Namna ya Kutoa Afua Stahiki |
|---|---|
| • Kuwa na vidonda au ukurutu mwilini<br>• Kuwa na utando mweupe mdomoni<br>• Kuwa na majipu<br>• Kuugua magonjwa nyemelezi<br>• Nywele kusimama au kukosa afya na rangi ya asili<br>• Viungo vya mwili kupooza<br>• Mpauko wa rangi ya mwili<br>• Kukohoa kusiko kwa kawaida<br>• Kasi kubwa ya mapigo ya moyo<br>• Kuvimba mwili au sehemu ya mwili<br>• Kupumua kwa haraka haraka au kwa shida<br>• Udumavu wa mwili | • Kuwapo kwa mazingira rafiki ya ujifunzaji<br>• Kutumia zana sahihi za ujifunzaji kwa Watoto wenye changamoto za kujongea<br>• Kutoa ushauri wa rufaa kwa matatizo yanayohitaji utaalamu zaidi, kwa mfano kuwapo kwa magonjwa kama vile kifafa, selimundu, saratani, VVU na UKIMWI<br>• Kutoa huduma za unasihi kwa watoto na wanafamilia na kutoa huduma ya kwanza inapohitajika<br>• Kuhamasisha wadau juu ya upatikanaji na utoaji wa lishe bora kwa watoto nyumbani na shuleni<br>• Kutoa motisha kwa kila hatua ya ujifunzaji |



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 59 15/04/2023 15:39

| Namna ya Kumtambua | Namna ya Kutoa Afua Stahiki |
|---|---|
| | • Kuonesha uvumilivu na upendo kwa watoto<br>• Kuzingatia uwezo na mahitaji yao katika ujifunzaji wao<br>• Ujifunzaji na ufundishaji uwe wa kurudiarudia<br>• Walezi na walimu kuwa na uangalizi wa karibu ili watoto wapate msaada wa haraka pale unapohitajika<br>• Kudumisha ujifunzaji unaozingatia mfumo wa elimu jumuishi<br>• Kuwe na mawasiliano mazuri kati ya wazazi na walimu ili kuweza kupeana taarifa kwa wakati zinazohusu maendeleo ya watoto wao |



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 60 15/04/2023 15:39

### 2.3.3.8 Kumtambua Mtoto mwenye Changamoto za Kijamii, Kihisia na Kitabia

Changamoto za kijamii, kihisia na kitabia ni hali changamani na sugu inayoathiri tabia, hisia, na uhusiano wa kijamii wa mtu.

Hali hii hutokana na athari mbalimbali zikiwamo za kufiwa na wazazi/walezi, magonjwa sugu, ugomvi wa kifamilia, ukosefu wa mahitaji ya msingi, unyanyaswaji na matukio ya majanga. Mtoto mwenye hali hii anaweza kutambuliwa kwa kuangalia tabia/dalili zilizoorodheshwa katika safu ya upande wa kushoto wa Jedwali Na. 11.

**Jedwali Na. 11: Kumtambua Mtoto mwenye Changamoto za Kijamii, Kihisia na Kitabia**

| Namna ya Kumtambua | Namna ya Kutoa Afua Stahiki |
|---|---|
| • Utukutu na ugomvi<br>• Ubishi na ghadhabu<br>• Kujiamini katika mazingira hatarishi<br>• Hofu, sonona, msongo wa mawazo, woga na kukata tamaa | • Onesha tabia ya upendo, kuwajali na kuwaelekeza kwa upole<br>• Wape motisha kila wanapoonesha kufanya vizuri |



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 61 15/04/2023 15:39

| Namna ya Kumtambua | Namna ya Kutoa Afua Stahiki |
|---|---|
| • Wepesi wa kuiga mambo mbalimbali yasiyofaa<br>• Hisia za kuonewa kila wakati<br>• Uongo, ukatili na kulipiza visasi<br>• Uharibifu wa vitu<br>• Lugha isiyo ya staha | • Wape kazi za vitendo kwa wingi<br>• Wape mazoezi ya kutosha na ya kufikirisha wakati wa kujifunza<br>• Washirikishe na hakikisha wanachangamana na watoto wengine katika kujifunza<br>• Wasikilize na kuwashauri namna ya kujifunza<br>• Wajengee uwezo katika stadi za maisha<br>• Wape huduma za unasihi na msaada wa kisaikolojia na kijamii<br>• Wape msaada wa ziada wakati wa kujifunza |

### 2.3.3.9 Kumtambua Mtoto mwenye Changamoto za Kipekee za Ujifunzaji

Changamoto za Kipekee za Ujifunzaji ni istilahi ya jumla ambayo inatokana na



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 62 15/04/2023 15:39

matatizo katika makuzi, uwezo wa kusikiliza, kutafsiri maelekezo, kuzungumza, kusoma, kuandika, kufikiri au kuhesabu.

Mtoto Mwenye Changamoto za Kipekee za Ujifunzaji anaweza kutambuliwa kupitia tabia/dalili zilizoorodheshwa katika safu ya upande wa kushoto wa Jedwali Na. 12.

**Jedwali Na. 12: Kumtambua Mtoto mwenye Changamoto za Kipekee za Ujifunzaji**

| Namna ya Kumtambua | Namna ya Kutoa Afua Stahiki |
|---|---|
| • Kushindwa kumudu stadi za kusikiliza, kujieleza, kusoma, kuandika, kuhesabu, na kutafsiri<br>• Kutumia ishara katika kujieleza<br>• Kutotulia na kukosa usikivu<br>• Kutomaliza kwa wakati kazi anazopewa<br>• Kuwa mtulivu wa kupitiliza<br>• Kujifunza polepole<br>• Kushindwa kujifunza baadhi ya stadi | • Kuwa mwangalifu wakati wa kutoa maelekezo Tumia maneno machache na tamka maneno kwa ufasaha na kwa kusikika<br>• Wape watoto mazoezi ya kutosha ya kusikiliza, kutamka kwa ufasaha, kuandika, kusoma na kuhesabu<br>• Hamasisha watoto kutumia lugha rasmi katika ujifunzaji<br>• Tumia mbinu ya ujifunzaji rika |



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 63 15/04/2023 15:39

| Namna ya Kumtambua | Namna ya Kutoa Afua Stahiki |
|---|---|
| • Kushindwa kujieleza na kutoa hisia zake kwa mtiririko mzuri<br>• Kutojiamini, aibu na kukata tamaa mapema<br>• Kushindwa kuwasiliana<br>• Kupendelea michezo ya hatari, muziki, na shughuli za vitendo zaidi<br>• Kutofuata maelekezo wanayopewa | • Shirikisha wazazi katika vitendo vya ujifunzaji vya mtoto<br>• Mpe fursa mtoto aongee mpaka amalize kisha mpe maelekezo sahihi<br>• Tumia mazingira halisi katika vitendo vya kujifunza<br>• Tumia nyimbo, hadithi, methali na michezo katika kujifunza (mbinu mwega)<br>• Toa ushauri wa rufaa inapobidi |

### 2.3.3.10 Kumtambua Mtoto mwenye Ulemavu wa Viungo

Ulemavu wa viungo ni hali ya kimaumbile inayoathiri uwezo wa kudhibiti mwendo wa misuli ambao mara nyingi huzuia ujongeaji. Ni dosari iliyopo kwenye viungo vya mwili ambayo husababisha viungo vilivyoathirika kutofanya kazi ipasavyo.



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 64 15/04/2023 15:39

Mfano wa dosari hizo ni kulemaa miguu au mikono. Hali hii husababishwa na ajali, magonjwa, na ukuaji duni wa mifupa, misuli na viungo vya mwili. Mtoto mwenye ulemavu wa viungo unaweza kumtambua kwa kuangalia tabia/dalili zilizoorodheshwa katika safu ya upande wa kushoto wa Jedwali Na. 13.

**Jedwali Na. 13: Kumtambua Mtoto mwenye Ulemavu wa Viungo**

| Namna ya Kumtambua | Namna ya Kutoa Afua Stahiki |
|---|---|
| • Ujongeaji wa mwili usio wa kawaida kwa mfano kutembea upandeupande<br>• Mjongeo wa mwili usio wa hiari<br>• Muonekano wa maumbile ya mwili yasiyo ya kawaida kwa mfano kibiongo<br>• Mguu au mkono kupooza<br>• Kushindwa kushika au kubeba vitu | • Kufanya vitendo vinavyochochea uchangamshi wa awali<br>• Kuhakikisha uwapo wa mazingira rafiki ya ujifunzaji<br>• Kutumia zana sahihi za ujifunzaji kwa watoto wenye changamoto za kujongea |



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 65 15/04/2023 15:39

| Namna ya Kumtambua | Namna ya Kutoa Afua Stahiki |
|---|---|
| • Kutumia vifaa saidizi kama vile gongo/ magongo, baiskeli ya magurudumu matatu na viungo vya bandia | • Kuwapatia watoto wenye changamoto za kujongea vifaa saidizi vya kujimudu kujongea, mfano magongo, viti vya magurudumu, na baiskeli za magurudumu matatu<br>• Kutoa ushauri wa rufaa kwa matatizo yanayohitaji utaalamu zaidi mfano uwapo wa magonjwa kama vile kifafa, selimundu, saratani, VVU na UKIMWI<br>• Kutoa huduma za unasihi kwa watoto na wanafamilia na kutoa huduma ya kwanza inapohitajika<br>• Kuhamasisha juu ya upatikanaji na utoaji wa lishe bora kwa watoto nyumbani na shuleni<br>• Kudumisha ujifunzaji unaozingatia mfumo wa elimu jumuishi |



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 66 15/04/2023 15:39

| Namna ya Kumtambua | Namna ya Kutoa Afua Stahiki |
| --- | --- |
| | • Kutoa motisha kwa kila hatua ya ujifunzaji<br>• Kuishirikisha jamii katika kutoa stadi za ujifunzaji kwa watoto wenye matatizo ya ujongeaji<br>• Kuonesha uvumilivu na upendo kwa watoto<br>• Kuwajengea watoto uwezo wa kumudu stadi za maisha<br>• Kuzingatia uwezo na mahitaji yao katika ujifunzaji wao<br>• Ujifunzaji na ufundishaji uwe wa kurudiarudia<br>• Kuwashirikisha wazazi katika kuwapa mazoezi ya viungo watoto wenye matatizo ya ujongeaji<br>• Walezi na walimu kuwa na uangalizi wa karibu ili watoto wapate msaada wa haraka pale unapohitajika |

| Namna ya Kumtambua | Namna ya Kutoa Afua Stahiki |
|---|---|
| | • Kuwe na mawasiliano mazuri kati ya wazazi na walimu ili kuweza kupeana kwa wakati taarifa zinazohusu maendeleo ya watoto wao |

Vifaa mbalimbali vinavyotumika kumtambua mtoto mwenye ulemavu wa viungo ni kama vile: rula, mpira, mkasi, kamba, chupa na mifuniko, rangi, na kalamu. Ili kumtambua kiwango cha utendaji wa viungo, mtoto aelekezwe kufanya yafuatayo:

i. Achore mistari kwa kutumia rula;
ii. Adake na arushe mpira;
iii. Akate vitu mbalimbali kwa kutumia mkasi;
iv. Aokote shanga na kuzitunga kwenye uzi;
v. Afungue na kufunga chupa;
vi. Apake rangi kwa kufuata mistari;
vii. Afunge na kufungua vishikizo vya nguo;
viii. Afunge kamba za viatu;
ix. Apange kibao fumbo;
x. Apange vibao jenga;



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 68 15/04/2023 15:39

xi. Apige mpira;
xii. Atembee kwa kufuatisha nyayo zilizochorwa sakafuni;
xiii. Atembee kwa kufuata mstari uliochorwa juu ya sakafu;
xiv. Asimame kwa mguu mmoja kwa sekunde nane (8); na
xv. Arukeruke juu mara tatu.

**Angalizo**: Mwalimu anapotumia vifaa hivi, ni vema azingatie kiwango na aina ya ulemavu wa viungo wa mtoto.

#### 2.3.3.11 Kumtambua Mtoto mwenye kufanyiwa vitendo vya ukatili

Ukatili nitendo lolote la makusudi la mtu au kikundi cha watu kumfanyia mtu mwingine kwa lengo la kumuumiza kimwili, kiakili au kifikra.

Ukatili dhidi ya watoto ni vitendo vya maksudi, vitisho au ushawishi unaofanywa na mtu au kikundi cha watu na kumsababishia mtoto madhara ya kimwili, kiafya au kisaikolojia.

Vitendo vya ukatili ni pamoja na mtoto kufanyishwa kazi ngumu, adhabu kali pamoja na adhabu za viboko zisizofuata utaratibu uliopo, unyanyasaji wa kijinsia, ukeketaji, mimba za utotoni pamoja na ndoa katika umri mdogo.



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 69 15/04/2023 15:39

**Jedwali Na. 14: Kumtambua Mtoto mwenye kufanyiwa vitendo vya ukatili**

| Namna ya kumtambua | Namna ya Kutoa Afua stahiki |
|---|---|
| • Kukosa usikivu kwa kuwa na mawazo mengi<br>• Woga na hasira<br>• Kupenda kujitenga na wengine<br>• Kushindwa kujieleza na kutumia ishara ya kukubali au kukataa<br>• Kuwa na msongo wa mawazo na kuishia kulia tu<br>• Kuwa mtulivu wa kupitiliza<br>• Kuwa na uso uliojawa na aibu na soni<br>• Kuonekana kwa michubuko na damu sehemu alizoshambuliwa<br>• Kutokwa na damu<br>• Kujisaidia kwenye nguo<br>• Kutembea mwendo tofauti na wengine<br>• Kuona alama za viboko | • Kuwa mwangalifu wakati wa kutoa maelekezo Tumia maneno<br>• machache na tamka maneno kwa ufasaha na yenye hekima<br>• Msikilize na mshawishi kuzungumza<br>• Toa ushauri kwa kutumia visa mafunzo<br>• Toa rufa kwa mtu mwenye stadi za ushauri na unasihi<br>• Shauriana na maafisa ustawi namna ya kutoa afua stahiki<br>• Kupewa huduma ya kwanza<br>• Kumpeleka hospitali<br>• Kuongea nae |



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 70 15/04/2023 15:39

### 2.3.4 Huduma ya Chakula na Lishe

Katika kutoa huduma ya lishe, unatakiwa kuzingatia mambo muhimu kadhaa, ikiwa ni pamoja na:

i. Kutoa vyakula vyenye virutubisho muhimu katika mazingira ya shule kulingana na umri wa watoto;
ii. Kuandaa ratiba ya utoaji wa huduma ya chakula shuleni;
iii. Kuandaa chakula katika mazingira safi na salama;
iv. Wapishi wapimwe afya katika vituo vya afya vinavyotambuliwa na serikali kabla ya kuajiriwa na warudiwe kila baada ya miezi sita;
v. Kuwe na stoo ya kuhifadhia chakula iliyo sehemu salama isiyo na unyevunyevu;
vi. Kuwe na chumba cha jiko kwa ajili ya kupikia pamoja na sehemu ya kulia chakula inayozingatia usalama wa watoto;
vii. Kuzingatia usafi na usalama wa vyombo vya chakula ili kuepuka magonjwa ya mlipuko;
viii. Kuwapo kwa sehemu safi na salama kwa ajili ya kuhifadhia vyombo vya chakula;
ix. Kuzingatia matumizi stahiki ya vyakula vilivyoongezwa virutubishi;
x. Kupunguza matumizi ya vyakula visivyoshauriwa kiafya kama vile mafuta, chumvi, na sukari kwa wingi ili kulinda afya za watoto; na



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 71 15/04/2023 15:39

xi. Kutumia maji tiririka au vitakasa mikono kabla na baada ya kula.

Kadhalika, chakula kinachotolewa kinapaswa kuwa salama kwa mtoto. Katika kuhakikisha usalama wa chakula, ni muhimu kuzingatia yafuatayo:

i. Kutathmini na kupima ubora wa chakula ili kukidhi viwango vya ubora na usalama wa chakula;

ii. Kuandaa na kuhifadhi vyakula katika mazingira safi na salama;

iii. Uhifadhi wa mbogamboga na matunda ufanyike bila kuathiri ubora wake;

iv. Uhifadhi wa chakula ufanyike kwa kuzingatia viwango vya uhifadhi vilivyoelekezwa na mamlaka inayohusika ili kuzuia uharibifu;

v. Kuteketeza chakula kilichoisha muda wake wa matumizi kwa kufuata utaratibu uliowekwa na Serikali; na

vi. Mazao ya chakula yahifadhiwe vizuri ili kuzuia uharibifu wa chakula na sumukuvu.

#### 2.3.4.1 Vifaa vya Chakula

Shule/ darasa la Elimu ya Awali linapaswa kuhakikisha kuwa vifaa vyote vya chakula vinapatikana na vinatunzwa katika hali ya



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 72 15/04/2023 15:39

usafi na usalama kuepusha matatizo ya kiafya kwa mtoto. Vifaa hivyo ni:

i. Sufuria za kupikia uji, chai na chakula;
ii. Miko ya kupikia;
iii. Sahani za kulia chakula;
iv. Vikombe vya kunywea chai au uji;
v. Vijiko vya kulia chakula;
vi. Maji safi na salama; na
vii. Mikeka, meza na viti vya watoto wakati wa kula.

### 2.3.4.2 Jiko

Suala la chakula na lishe kwa watoto ni muhimu kulipa kipaumbele ili kutengeneza mazingira rafiki katika kujifunza. Ili kufanikisha mchakato huu, lazima shule iwe na eneo la kuandalia chakula ambalo litakuwa na jiko la kupikia, vyombo, maji na chakula kwa ajili ya watoto. Shule na wadau wanapaswa kuzingatia yafuatayo:

i. Usafi na usalama katika jiko la kupikia;
ii. Jiko liwe mbali kidogo na madarasa;
iii. Kuwe na madirisha makubwa ya kupitisha hewa ili kuruhusu mzunguko



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 73 15/04/2023 15:39

mzuri wa hewa; na

iv. Kuwe na vyombo stahiki vya kupikia kama vile sufuria na mwiko.

#### 2.3.4.3 Maji

Maji ni muhimu sana katika ustawi wa afya za watoto, walimu na wadau wanaoizunguka shule. Uongozi na wadau wanapaswa kuhakikisha kuwa na chanzo cha uhakika katika upatikanaji wa maji safi na salama kama vile bomba, kisima, na tenki kulingana na huduma zitolewazo shuleni.

### 2.3.5 Miundombinu Stahiki

Katika kuboresha mchakato wa makuzi na ujifunzaji wa watoto wa Elimu ya Awali, shule au madarasa ya awali yawe katika sehemu iliyo rahisi kufikika kwa watoto wote. Madarasa yasiwe ghorofani, karibu na viwanda, karibu na stoo, baa, duka au hata sehemu yoyote hatarishi. Shule/darasa linatakiwa kuwa na miundombinu inayoweza kuchochea ari ya ufundishaji na ujifunzaji ili kufikia malengo yaliyokusudiwa kwa watoto. Miundombinu hiyo ni kama vile vyumba vya madarasa, vyoo, viwanja vya michezo, jiko la kupikia, na maji.



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 74 15/04/2023 15:39

#### 2.3.5.1 Vyumba vya Madarasa

Darasa la Elimu ya Awali ni darasa lisilokuwa na kuta wala paa ambalo hujumuisha watoto wenye mahitaji tofauti ya ujifunzaji ili mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, uwe na ufanisi kwa watoto kujifunza, unatakiwa kuhakikisha mambo yafuatayo:

i. Kuzingatia uwiano wa watoto katika darasa uwe 1:25;
ii. Kuwapo kwa vyumba viwili (darasa la mwanzo na darasa la maandalizi);
iii. Kuwapo kwa chumba kikubwa chenye hewa na mwanga wa kutosha;
iv. Kuwapo kwa chumba cha mapumziko na kinachoweza kutumika kama chumba cha masuala ya afya;
v. Kiwe na nafasi kubwa kuruhusu vitu kuonekana vizuri wakati wa kujifunza;
vi. Kuandaa darasa linaloongea, lenye machapisho na zana mbalimbali zinazozingatia muktadha wa ujifunzaji;
vii. Kuwapo kwa kona za ujifunzaji zitakazoimarisha maarifa kwa mtoto na kukuza stadi mbalimbali, zikiwamo za kusoma, kuandika, na kuhesabu;

Kona hizo ni kona ya hisabati, sayansi, nyumbani, sanaa, dukani, lugha (kusoma na kuandika). Aidha, kona ya nje ijumuishe pia eneo la michezo pamoja na eneo la mchanga na maji; na

viii. Ujumuishi unaozingatia mahitaji ya kila mtoto ili waweze kujifunza kwa usawa.

### 2.3.6 Huduma ya Vyoo

Shule/darasa la Elimu ya Awali linatakiwa kuwa na huduma ya vyoo kulingana na mahitaji ya watoto ili kusaidia afya na ustawi wa watoto. Uongozi wa shule uhakikishe matundu ya vyoo yanaendana na umri na idadi ya watoto kwa kuzingatia yafuatayo:

i. Wastani wa tundu 1 kwa watoto wa kike 20 na tundu 1 kwa watoto wa kiume 25;

ii. Vyoo vinavyozingatia hali ya watoto wenye mahitaji maalumu, tundu 1 kwa watoto wa kike na tundu 1 kwa watoto wa kiume. Idadi ya matundu ya vyoo itaongezeka kulingana na idadi ya wanafunzi;

iii. Uwapo wa kibuyu chirizi au maji tiririka ya kunawa na sabuni; na

iv. Usafi na usalama nje na ndani ya vyoo.

### 2.3.7 Viwanja vya Michezo

Haya ni maeneo maalumu yanayotumika katika michezo na kuchochea ujifunzaji wa mtoto. Viwanja viwe na nafasi ya kutosha kwa ajili ya kuwapa uhuru watoto katika kucheza na kujifunza. Viwanja ni kama vile viwanja vya mpira wa miguu, mpira wa pete, mpira wa mikono, kuruka kamba, na dama.

Mambo ya kuzingatia unapoandaa viwanja vya michezo:

i. Kuangalia mahitaji ya watoto kiafya na kimwili ili kurahisisha ushiriki wa kila mtoto wakati wa kucheza;

ii. Kuondoa vitu hatarishi katika maeneo ya viwanja ili kupunguza ajali kwa watoto wakati wa kucheza (visiki, mawe, chupa zilizovunjika, vijiti na vitu vyenye ncha kali);

iii. Kuwe na ujumuishi ili kuruhusu kila mtoto kushiriki kulingana na hali yake;

iv. Kuzingatia vipimo vinavyoendana na umri na uwezo wa watoto kwa mchezo husika; na

v. Vifaa vya michezo kwa watoto wenye mahitaji maalumu viongezwe. Mpira wenye kengele, mpira wenye miba (thorn ball), mpira laini, shanga zenye ukubwa tofauti na zenye rangi tofauti na filimbi.



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 77 15/04/2023 15:39

### 2.3.8 Vifaa na Samani

Darasa la Elimu ya Awali linapaswa kuwa na vifaa na samani ambavyo vitatumiwa na mwalimu pamoja na watoto katika kurahisisha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Kuwapo kwa vifaa shuleni/darasani huwezesha mazingira rafiki ya kujifunzia kwa watoto. Miongoni mwa vifaa vinavyoweza kutumika katika darasa la Elimu ya Awali ni zana za kufundishia na kujifunzia, samani, vifaa vya michezo, vifaa vya chakula, na sanduku la huduma ya kwanza.

Samani, midoli na vifaa vingine wanavyotumia watoto katika ujifunzaji kwa njia ya michezo vinapaswa kutunzwa katika hali salama, safi, na nzuri kiafya. Suhula zinazoweza kusababisha ajali au kuhatarisha usalama wa watoto zinapaswa kutupwa mara moja, kurekebishwa au kuwekwa mbali na upeo wa watoto.

Tahadhari zinapaswa kuchukuliwa ili kuhakikisha kuwa samani na vifaa vyote viko salama, bila kuwapo na vitu vyenye ncha kali iliyochongoka kama vile misumari inayojitokeza kuweza kuhatarisha maisha ya watoto. Katika ununuzi wa suhula na vifaa vya ujifunzaji, ni lazima kuhakikisha usalama wa watoto umezingatiwa.



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 78 15/04/2023 15:39

Aidha, watoto wasiruhusiwe kupanda juu ya fremu za dirisha au kucheza karibu na madirisha kuepusha hatari zinazoweza kujitokeza.

### 2.3.9 Vifaa vya Michezo ya Ndani na Nje

Kuwapo kwa mwalimu na msaidizi wa mwalimu ili kusimamia watoto kucheza pamoja na:

i. Vifaa vya michezo ya kujenga mwili kwa watoto kutumika kwa uangalifu pamoja na kuwapo kwa usimamizi wa karibu kutoka kwa mwalimu au msaidizi wa mwalimu;
ii. Kuweka tahadhari kutokana na hali ya hewa na hali ya afya ya watoto kwa kuzingatia shughuli zinazofanyika nje na mbali na upeo wa msimamizi.
iii. Maelekezo ya wazi na ya kina yanapaswa kutolewa kwa watoto kabla ya kila shughuli;
iv. Vifaa vya kucheza vinapaswa kuwa imara, kuchunguzwa mara kwa mara, na kudumishwa. Ili kuhakikisha usalama, vifaa vinapaswa kuchunguzwa kila mara kabla ya matumizi na kutunzwa sehemu salama; na
v. Vifaa vikubwa vikiwamo vya kubembea, kuteleza, na kuruka vikwazo, vinahitaji eneo kubwa lenye nafasi ya kutosha.


KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 79 15/04/2023 15:39

Mwalimu unapaswa kuhakikisha vifaa vyote muhimu vya michezo vinapatikana ili kuwasaidia watoto kukuza stadi za awali za kusoma, kuandika na kuhesabu. Baadhi ya vifaa anavyopaswa kuviandaa mwalimu wa darasa la awali ni:

i. Mipira, bembea, kamba, dadu, vibao, vijiti, kadi, vifuniko vya chupa, kokoto na matairi;
ii. Vifaa vya kufundishia utamkaji wa sauti na maneno (saka neno) kwa ajili ya kujifunzia stadi za awali za KKK;
iii. Vifaa vya michezo ya nje kama sehemu ya kuwachangamsha watoto;
iv. Mavazi ya kuigizia ili kuwasaidia watoto kukuza stadi za kisanii; na
v. Ngoma (seti ya ngoma) za kutumia katika kuwafundisha watoto stadi za muziki na utamaduni.

Mafunzo elekezi yanapaswa kutolewa kwa watoto kuwasaidia kukuza ufahamu na kuweka tahadhari ili kuhakikisha usalama wao wenyewe na wa wengine wanaocheza nao. Vilevile, watoto wanapaswa kukumbushwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu kama ifuatavyo:

i. Watoto wanapaswa kuwa mbali na mazingira hatarishi wakati wa shughuli za kikundi nje ya darasa;



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 80 15/04/2023 15:39

ii. Watoto wanapaswa kuwa na adabu wakati wote katika mchezo na kutumia vifaa vya michezo ipasavyo kwa usimamizi wa mwalimu au msaidizi wa mwalimu;
iii. Kuwe na uangalizi wa watoto wakati wa kukimbia, kuruka na kucheza michezo ya vikwazo;
iv. Shule ziweke mipaka ya eneo la michezo ya nje, mfano kuzunguka eneo la bembea; na
v. Watoto waelekezwe kuhusu alama za tahadhari.

### 2.3.10 Zana za Kujifunzia na Kufundishia

Wakati wa kuwawezesha watoto, walimu wanatakiwa kumjengea mtoto uwezo kwa kutumia zana kwa ajili ya kujenga, kufafanua, kubainisha na kuchakata dhana anayojifunza ili kufikia umahiri uliokusudiwa. Walimu, kwa kushirikiana na jamii na wadau mbalimbali, wanatakiwa kuhakikisha zana za kufundishia na kujifunzia darasa la Elimu ya Awali zinapatikana. Katika kutumia zana, mambo muhimu ya kuzingatia ni:

i. Kuangalia umri na uwezo wa watoto katika kutumia zana kutekeleza shughuli za ujifunzaji;



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 81 15/04/2023 15:39

ii. Kutumia zana ambazo hazisababishi madhara kwa watoto;

iii. Kutumia zana zinazojenga udadisi unaoibua fikra tunduizi ili kukuza stadi za ubunifu, ushirikiano, na mawasiliano;

iv. Kuandaa zana zinazolenga kuwashirikisha watoto wote, na kuwajumuisha hata wenye mahitaji maalumu katika kujifunza; na

v. Kujenga dhana iliyokusudiwa wakati wa kutekeleza mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.

### 2.3.11 Vifaa vya Huduma ya Kwanza

Wakati wa utekelezaji wa shughuli za ufundishaji na ujifunzaji, kunaweza kutokea ajali tofauti kwa watoto kama vile kuumia, kuumwa na wadudu, na kujijeruhi. Mwalimu anapaswa kuwa na sanduku la Huduma ya Kwanza ili kuweza kuwapatia watoto huduma ya kwanza. Sanduku la huduma ya kwanza linapaswa kuwa na dawa za kusaidia kuondoa maumivu, spiriti, ayodini, yuso, bandeji, mkasi, viwembe, vifaa kinga, na pamba.



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 82 15/04/2023 15:39

# SEHEMU YA TATU

## UPIMAJI WA MATOKEO YA UJIFUNZAJI

### 3.1 Utangulizi

Sehemu hii inafafanua upimaji wa maendeleo ya mtoto wa Elimu ya Awali. Kwa kawaida, upimaji katika ngazi hii hufanyika kwa kuzingatia vitendo vya mtoto hatua kwa hatua na kubaini viashiria vya matokeo ya utendaji ili kujua kiwango alichofikia. Aidha, upimaji wa maendeleo ya mtoto hufanyika kwa kufuatilia mabadiliko ya ukuaji na ujifunzaji ili kubaini stadi zinavyoendelea kuibuka kutokana na ujifunzaji wa mtoto ukilinganisha na hatua zake za makuzi. Hivyo, upimaji wa matokeo ya ujifunzaji utakuwa na ufanisi zaidi ikiwa michezo ya utendaji itatumika katika upimaji badala ya kutumia mitihani ya ulinganifu.

Upimaji huu wa kutumia michezo ya utendaji unalenga kubaini kiwango cha ujifunzaji wa mtoto, stadi zilizoibuliwa, stadi zilizojengwa na zile zinazotakiwa kuendelezwa. Upimaji huu huzingatia mambo ambayo mtoto amejifunza, uzoefu wake, na mahitaji yake kulingana na umri na hulenga vitendo kutoka katika umahiri wa kuhusiana, kuwasiliana, kutunza afya, kutunza mazingira, kumudu stadi za kisanii na kumudu dhana za kihisabati.



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 83 15/04/2023 15:39

Michezo ndiyo nyenzo kuu ya mtoto kwa sababu anapocheza, anajifunza, na anapojifunza, na anacheza hivyo, upimaji wa matokeo ya ujifunzaji wa mtoto wa Elimu ya Awali utategemea zaidi michezo ya utendaji kubaini kiwango cha utendaji kilichofikiwa.

Sura hii inatoa maelekezo kwa mpimaji kuhusu namna ya kutumia maswali dodoso na kumhamasisha mtoto kucheza michezo inayoendana na shughuli tendwa ili aweze kupima matokeo ya ujifunzaji wa mtoto huyo. Aidha, sura inaelekeza namna ya kuweka alama kwa kila swali kwa kuzingatia maelekezo ya kila swali. Kwa hiyo maswali dodoso yatakuwezesha kupima maendeleo ya ujifunzaji wa watoto wenye umri kati ya miaka 3 - 5 kulingana na mahitaji ya kila mtoto. Hatua zote tatu za upimaji, ambazo ni upimaji wa awali, endelevu na tamati zimezingatiwa. Hivyo, unapaswa kuzingatia maelekezo yaliyotolewa, kuandaa vifaa/zana zinazohitajika wakati wa upimaji pamoja na kumsomea mtoto maswali kwa usahihi.

## 3.2 Namna ya Kupima Viwango vya Utendaji

Upimaji wa matokeo ya ujifunzaji unatakiwa kuzingatia viashiria vya utendaji ili kupata matokeo tarajiwa. Weka alama ya vema mara baada ya kupima matokeo ya utendaji kwa njia ya mchezo ulioouchagua.



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 84 15/04/2023 15:39

Ufikapo mwisho wa upimaji, tenga muda kuhakikisha kuwa kila swali limewekewa alama ili kujumlisha alama hizo. Kisha, jumla ya alama hizo gawa kwa idadi ya maswali ili kupata wastani. Zingatia viwango vya utendaji vilivyofikiwa katika umahiri husika kama ifuatavyo:

*i.* ***Hajaweza*** inamanisha kuwa mtoto hajaonesha stadi iliyokuwa inapimwa;

*ii.* ***Wastani*** inamanisha kuwa mtoto amejaribu kwa kiasi kidogo kuonesha stadi iliyokuwa inapimwa;

*iii.* ***Vizuri*** inamanisha kuwa mtoto ameonesha stadi iliyokuwa inapimwa kwa kiwango cha kati; na

*iv.* ***Vizuri sana*** inamanisha kuwa mtoto ameonesha stadi iliyokuwa inapimwa kwa kiwango cha juu.

Ili kuvitumia viwango hivi vizuri na kwa ufanisi, unashauriwa kutumia kiongozi cha upimaji cha kila umahiri, ambapo viashiria vya utendaji vimeelekezwa kwa kila swali/mchezo.

### 3.2.1 Maandalizi ya Kufanya Upimaji

Kabla ya kuanza upimaji wa matokeo ya ujifunzaji unapaswa kufanya maandalizi ya mtoto. Hii itasaidia kujua utayari wake kwa ajili ya zoezi la upimaji kabla ya kuanza upimaji.



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 85 15/04/2023 15:39

Andaa vifaa vya upimaji, vikiwamo vijarida vya vitendo changamshi vya mtoto, suhula za kufanyia uchangamshi na zana stahiki zitakazotumika pamoja na mchezo ambazo ni orodha hakiki na mkoba wa kazi. Rejea kiongozi cha ufundishaji wa Elimu ya Awali kinachotumika na vitabu vya rejea katika malezi, makuzi na maendeleo ya mtoto. Endapo wewe ni mpimaji ambaye si mwalimu katika shule husika, utalazimika kuomba ridhaa katika mamlaka husika kabla ya kufanya zoezi hilo.

### 3.2.2 Mazingira ya Kufanyia Upimaji

Upimaji wa matokeo ya ujifunzaji unatakiwa ufanyike katika mazingira tulivu yanayohusu ujifunzaji. Kabla ya kuanza kupima, hakikisha kuwa mazingira ni salama na tulivu na hakuna mwingiliano wa watu na vitu ambavyo vinaweza kusababisha mtoto asiwe na usikivu. Aidha, unatakiwa kujenga mazingira ya kirafiki na mtoto kwa kumuuliza maswali kuhusu michezo anayopenda kuicheza au kitu kingine kinachomfurahisha katika mazingira aliyopo. Kwa kifupi, mfanye mtoto ajue kwamba kinaendelea kufanyika ni micxhezo badala ya mtihani.



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 86 15/04/2023 15:39

### 3.2.3 Mambo Muhimu ya Kuzingatia katika Upimaji

Ili upimaji ufanyike kwa ufanisi, yafuatayo ni mambo muhimu ya kuzingatia:

i. Lengo la upimaji;
ii. Mtaala wa Elimu ya Awali;
iii. Mwongozo wa Mwalimu wa kufundishia Elimu ya Awali;
iv. Mahitaji ya mtoto;
v. Zana za upimaji;
vi. Kiongozi cha Upimaji katika Elimu ya Awali kwa kutumia michezo; na
vii. Fomu ya makuzi na maendeleo ya mtoto.

Mwelekeze mtoto namna ya kuanza kucheza, mwoneshe tabasamu na umweleze nini cha kufanya. Anza kutambulisha mchezo na kufuata maelekezo hatua kwa hatua. Soma vizuri maelekezo katika mwongozo wa mpimaji, kisha mpe mtoto kifaa chake kinachoonesha vitendo vya michezo iliyopendekezwa. Upimaji umegawanyika katika makundi matatu: upimaji wa awali, endelevu na tamati.

### 3.2.4 Umahiri Unaokusudiwa Kupimwa

Upimaji huu utafanyika katika umahiri wa aina zote kulingana na Muhtasari wa Elimu ya Awali ambazo ni umahiri wa kuhusiana, kuwasiliana,



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 87 15/04/2023 15:39

kutunza afya, kutunza mazingira, kutumia dhana za kihisabati na kumudu stadi za kisanii.

### Umahiri wa Kuhusiana

Umahiri huu unahusisha mabadiliko ya mtoto kitabia, kiuhusiano, utayari katika kutenda na kuiga, kushirikiana, kuthamini utu wake na wa watu wengine na kuthamini vitu vilivyoko katika mazingira, kuonesha uvumilivu, uzalendo na kuwa na mtazamo chanya. Upimaji katika umahiri huu hufanyika katika vitendo vya kusalimiana, kutambulishana, kushiriki katika kazi mbalimbali, uwezo wa kusaidia watu wengine, uwezo wa kujitawala na kumudu mazingira yake, uwezo wa kujitegemea, na tabia ya kutunza vitu.



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 88 15/04/2023 15:39

**Jedwali Na. 15: Kumudu Stadi za Awali za Kuhusiana**

| Kipengele | Kigezo | Kiashiria |
|---|---|---|
| **Kujitambua** | Kujithamini na kuthamini wengine (kujitambua) | • Anajijali mwenyewe<br>• Anawajali watu wengine<br>• Anatambua jinsi yake<br>• Anajitambulisha<br>• Anatambulisha watu wengine<br>• Anaonesha ushirikali<br>• Anaheshimu tofauti iliyopo miongoni mwa watu wanaomzunguka |
| **Kutawala hisia** | Kutawala hisia katika miktadha mbalimbali | • Anatambua hisia, mawazo na matendo ya watu wengine<br>• Anaonesha uvumilivu anapotofautiana na wenzake |



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 89
15/04/2023 15:39

| Kipengele | Kigezo | Kiashiria |
|---|---|---|
| | | • Anaeleza hisia zake<br>• Anajivunia pale anapofanya vizuri katika jambo fulani |
| **Kujitegemea** | Kumudu stadi za kujitegemea | • Ana uwezo wa kwenda chooni mwenyewe<br>• Anavaa na kuvua nguo/soksi/viatu mwenyewe<br>• Anapanga vitu katika utaratibu unaotakiwa<br>• Anajiamini katika wakati tofauti |
| **Kushirikiana** | Kumudu stadi za Kushirikiana | • Ana uwezo wa kushirikiana na wenzake katika michezo<br>• Anatambua kuwa matendo yake yanaathiri wengine katika hali ya uchanya na hasi |



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 90
15/04/2023 15:39

| Kipengele | Kigezo | Kiashiria |
| --- | --- | --- |
| | Kutatua changamoto katika maisha ya kila siku | • Anasuluhisha panapotokea tatizo<br>• Anaenda na muda<br>• Anaomba na anapokea msaada kwa watu wengine<br>• Anawashirikisha wengine |



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 91 15/04/2023 15:39

## Umahiri wa Lugha na Kuwasiliana

Umahiri wa kuwasiliana humwezesha mtoto kukua kiakili, kijamii, na kihisia. Katika umahiri huu, upimaji wa matokeo ya ujifunzaji utafanyika katika stadi zifuatazo:

i. Stadi ya kusikiliza humwezesha mtoto kujenga usikivu kwa kusikiliza vitu vinavyotoa sauti na milio. Upimaji wa stadi hizi utafanyika ili kupima kiwango cha utendaji wa mtoto katika kubaini na kutofautisha sauti na milio. Aidha, kwa kutumia mbinu ya hadithi, mtoto ataweza kutaja wahusika na kueleza ujumbe. Vilevile, mtoto atapimwa kuona kama anaweza kusikiliza maelekezo au maagizo na kutenda ipasavyo. Afua stahiki zitatolewa kwa wenye changamoto zitokanazo na usikivu hafifu pamoja na kushindwa kutofautisha sauti na milio kulingana na hatua za ujifunzaji;

ii. Stadi ya kuzungumza hukuza uwezo wa mtoto wa kuwasiliana, kujenga uhusiano, kujiamini, na kujifunza kwa urahisi. Upimaji katika umahiri huu utafanyika ili kupima kiwango cha utendaji wa mtoto kutamka sauti za herufi katika silabi, maneno, sentensi kuwa na ushikamani, na lafudhi sahihi na kiimbo katika maneno au sentensi. Matokeo ya upimaji yatawezesha kutoa afua stahiki kwa watoto wenye changamoto za kuzungumza pamoja na umaliziaji wa maneno ili yalete maana:



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 92 15/04/2023 15:39

iii. Stadi za awali za kusoma hujengeka kabla mtoto hajaanza kusoma rasmi. Stadi hizi humwezesha mtoto kujenga uwezo wa kuwasiliana katika mambo mbalimbali. Upimaji katika stadi hii utafanyika ili kupima kiwango cha utendaji katika stadi za awali za kusoma kwa kufuata hatua stahiki, kasi stahiki, pamoja na utamkaji wa maneno kwa usahihi. Aidha, mtoto atapimwa ili kuona namna anavyoshika machapisho, kufuatilia picha na kupata maudhui; na

iv. Stadi za awali za kuandika zinazohusisha uwezo wa mtoto kuwasiliana kwa njia ya maandishi. Upimaji katika stadi hii huhusisha mkao sahihi wakati wa kuandika, namna ya kushika viandikia, mkono sahihi anaotumia wakati wa kuandika, ambapo mwelekezaji anatakiwa kuwa katika upande sahihi ili amwelekeze mtoto namna ya kuandika. Vilevile, upimaji huhusisha kushika kiandikio kwa vidole vitatu (gumba, shahada na kati); kuachia inchi moja kutoka ncha ya kiandikio mpaka vidole vinapoanzia; kuegemea kwenye dawati au meza wakati wa kuandika; na kuweka sehemu ya juu ya tumbo ikaribie kugusa dawati au meza na si kuinamia upande mmoja.

Mpimaji anatakiwa awe upande sahihi kutokana na matumizi ya mkono, mfano kama mtoto anatumia mkono wa kushoto, mguu wa kulia utakanyaga mwamba wa chini kwenye dawati na mkono wa kulia uwe juu ya dawati



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 93 15/04/2023 15:39

katika alama ya (V), angalau nyuzi 45 kuelekea sehemu ya juu ya kibao au daftari la mtoto. Ikiwa anatumia mkono wa kulia, mguu wa kushoto utakanyaga mwamba wa chini kwenye dawati na mkono wa kushoto uwe juu ya dawati katika alama ya (V), angalau nyuzi 45 kuelekea sehemu ya juu ya kibao au daftari la mtoto.

Hatua za kufuata kumwelekeza mtoto namna ya kuandika ni pamoja na:

i. Kuonesha michoro hewani jinsi ya kuandika mchoro/herufi hewani akiwa amesimama;

ii. Kuandika mchangani/ardhini kwa kutumia kidole au kijiti;

iii. Kuandika kwenye vibao ambazo ni mwendelezo wa hatua zilizotangulia;

iv. Mtoto aandike kwa kutumia vibao na viandikio kadri ya aina ya vibao; na

v. Kuandika kwenye daftari kwa kalamu kuzingatia mkao sahihi na ushikaji mzuri wa kalamu.

Zingatia uumbaji wa herufi kwa kuwawezesha watoto kuanza na daftari lisilo na mistari ili kumpa mtoto uhuru wa kujifunza kuandika maumbo mbalimbali. Baadaye, mtoto atumie daftari la mistari yenye nafasi pana na nyembamba ili kumwongoza vema kuumba herufi mbalimbali akianza na herufi za irabu, kisha konsonati kwa kuzingatia makundi yake. Zifuatazo ni hatua za uumbaji wa herufi:



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 94 15/04/2023 15:39

i. Kuandika michoro mama yenye kurahisisha uumbaji wa herufi mbalimbali;
ii. Kuandika herufi kwa kuzingatia hatua tofauti za uumbaji wa kila herufi;
iii. Kuandika silabi; na
iv. Kuandika maneno.

**Namna ya Kuumba Herufi**

Mtoto aelekezwe namna ya kuumba/kuandika herufi kwa kuzingatia herufi zinazoandikwa kwa kutembeza mkono bila ya kunyanyua kiandikio wakati wa kuumba herufi ambazo ni a, b, t, e, g, h, l, m, n, o, p, r, s, u, v, w, y, z. Aidha, kuna herufi ambazo huandikwa kwa kunyanyua mkono. Herufi hizo ni l, ch, j, k, na t.



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 95 15/04/2023 15:39

**Jedwali Na. 16: Kumudu Stadi za Awali za Lugha na Mawasiliano**

| Kipengele | Kigezo | Kiashiria |
|---|---|---|
| **Kusikiliza** | Kusikiliza katika miktadha mbalimbali | Mwitikio wa mtoto:<br>• Anaonesha mwitikio<br>• Anatofautisha sauti na milio,<br>• Anauliza maswali ya kufikirisha kwa mfano: kwa nini?, kwa vipi?, ingekuwaje?<br>• Anafuata maelekezo na maagizo<br>• Anaelezea ujumbe kutokana na habari aliyosikia<br>• Anaigiza matendo ya wahusika<br>• Anaelezea ujumbe kutokana na habari aliyosikia<br>• Anaigiza matendo ya wahusika |



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 96 15/04/2023 15:39

| Kipengele | Kigezo | Kiashiria |
|---|---|---|
| | | • Anaelezea vitu anavyovipenda na asivyovipenda<br>• Anatamka maneno aliyoyazoea zaidi katika lugha ya Kiswahili |
| **Kuzungumza** | Kuzungumza katika miktadha mbalimbali | • Anazungumza kwa kujiamini mbele ya wenzake<br>• Anasimulia hadithi<br>• Anabashiri tukio linaloweza kutokea<br>• Anatamka maneno kwa ufasaha<br>• Anaongea sentensi iliyokamilika |



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 97
15/04/2023 15:39

| Kipengele | Kigezo | Kiashiria |
|---|---|---|
| **Kusikiliza** | | Mwitikio wa mtoto katika kuelezea matukio anayoyafanya |
| **Kusoma** | Kusoma katika hatua za awali | • Anatembeza macho kutoka kushoto kwenda kulia<br>• Anatembeza macho kuanzia juu kwenda chini<br>• Anasoma picha<br>• Anasoma sauti za herufi za irabu (a, e, i, o, u)<br>• Anasoma sauti za herufi za konsonanti (b, m, k, d, n), (l, t, p, s, f, j), g, y, z, h, r, w, v, ch)<br>• Anashika kitabu kwa usahihi<br>• Anasoma majina ya herufi |



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 98 15/04/2023 15:39

| Kipengele | Kigezo | Kiashiria |
|---|---|---|
| | | • Anahusianisha jina na sauti ya herufi<br>• Anasoma silabi<br>• Anasoma maneno mafupi ambayo si mwambatano na yasiyokuwa na ving'ong'o |
| **Kuandika** | Kuandika katika hatua mbalimbali | • Anatembeza mkono kutoka kushoto kwenda kulia<br>• Anashika viandikia kwa kutumia vidole stahiki<br>• Anafuata hatua za uumbaji wa herufi<br>• Anaandika herufi za irabu na konsonanti<br>• Anaandika silabi |



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 99 15/04/2023 15:39

| Kipengele | Kigezo | Kiashiria |
|---|---|---|
| | | • Anaandika maneno mafupi yasiyozidi silabi tatu<br>• Anaandika sentensi fupi isiyozidi maneno mawili |
| **Kuwasiliana** | Kuwasiliana katika miktadha mbalimbali | • Anazungumza lugha ya Kiswahili kwa ufanisi<br>• Anatumia lugha ya alama ya Tanzania katika kuwasiliana<br>• Anatumia lugha ya mguso katika kuwasiliana<br>• Anatumia maandishi ya Breili katika kuwasilisha taarifa kwa maandishi |



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 100
15/04/2023 15:39

## Umahiri wa Kutunza Afya

Sehemu hii inalenga kumwezesha mtoto kujenga uwezo wa kutunza afya. Upimaji wa mtoto utahusisha mabadiliko ya mtoto yanayotokana na vitendo anavyofanya katika kubainisha sehemu za nje za mwili wa binadamu, kutumia vifaa vya kufanyia usafi wa mwili, mavazi na namna anavyoyatumia mazingira yake kujifunza. Mambo mengine ni pamoja na kutambua chakula bora, kubaini magonjwa na vyanzo vyake, na jinsi ya kujikinga na magonjwa hayo.



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 101 15/04/2023 15:39

**Jedwali Na. 17: Kumudu Stadi za Kutunza Afya**

| Kipengele | Kigezo | Kiashiria |
|---|---|---|
| **Kutunza afya ya mwili** | Kutunza mwili ili kuwa na afya njema | • Anabaini vifaa vya usafi wa mwili (mswaki, dawa ya meno, kitambaa laini, sabuni, maji, beseni, taulo, dodoki, kikata kucha na kopo la kuchotea maji)<br>• Ana urazini wa kufanya usafi wa mwili |
| **Kula vyakula mbalimbali** | Kuthamini vyakula vya aina mbalimbali | • Anataja aina za vyakula mbalimbali<br>• Anakula vyakula<br>• Anachora vyakula anavyovipenda<br>• Anataja vifaa vinavyotumika kusafishia vyombo<br>• Anasafisha vyombo |



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 102
15/04/2023 15:39

| Kipengele | Kigezo | Kiashiria |
|---|---|---|
| **Kutunza vyombo** | Kuchukua tahadhari dhidi ya magonjwa mbalimbali | • Anataja sehemu zinazotumika kutunza vyombo<br>• Anaonesha matumizi stahiki ya vyombo<br>• Anataja magonjwa mbalimbali<br>• Anabaini vyanzo vya magonjwa<br>• Anaeleza jinsi ya kujikinga na magonjwa |
| | Kuchunguza vitu vilivyopo katika mazingira | • Anabaini vitu vilivyomo katika mazingira |
| | Kusafisha mazingira | • Anataja vifaa vya kufanyia usafi<br>• Anaonesha urazini wa kusifisha mazingira |



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 103
15/04/2023 15:39

## Umahiri wa Kutunza Mazingira

Mazingira ni jumla ya vitu vyote vinavyomzunguka mwanadamu, ikiwa ni pamoja na wanyama na mimea. Umahiri wa kutunza mazingira utamwezesha mtoto kujenga uwezo kuyapenda, kuyajali, kuthamini na stadi za kutunza mazingira. Upimaji wa umahiri huu utahusisha vitendo mbalimbali vya utunzaji wa mazingira kwa mtoto, ikiwa ni pamoja na uwezo wa kutambua vitu katika mazingira yake, kusafisha mazingira, kubaini vitu vinavyochafua mazingira, kubaini vitu na maeneo hatarishi, na kuchukua tahadhari.



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 104 15/04/2023 15:39

**Jedwali Na. 18: Kumudu Stadi za Kutunza Mazingira**

| Kipengele | Kigezo | Kiashiria |
|---|---|---|
| **Urazini wa mazingira** | Kuchunguza vitu vilivyopo katika mazingira | • Anabaini vitu vilivyomo katika mazingira |
| | Kusafisha mazingira | • Anataja vifaa vya kufanyia usafi<br>• Anaonesha urazini wa kusafisha mazingira |
| **Kuchukua tahadhari** | Kuchukua tahadhari katika mazingira | • Anataja alama za tahadhari<br>• Anatambua mazingira hatarishi<br>• Anaeleza namna ya kuchukua tahadhari<br>• Anatenda matendo yanayohusisha kuchukua tahadhari<br>• Anaomba msaada kwenye mazingira hatarishi |



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 105
15/04/2023 15:39

**Umahiri wa Kumudu Stadi za Kisanii, Ubunifu na Michezo**

Umahiri huu wa stadi za Sanaa ni jumla ya mambo yote yanayofanywa na mwanadamu kwa ufundi au ubunifu na kwa kuzingatia ujumi unaojitokeza ili kuleta uhalisia. Katika eneo hili, mtoto atawezeshwa kumudu Sanaa za ubunifu zinazohusisha utendaji wa mikono na mwili na kumudu Sanaa za ubunifu wa sauti. Upimaji wa umahiri huu utafanyika kwa kutumia stadi za ubunifu wa utendaji wa mikono, kuumba maumbo, kuchora picha, kupaka rangi na nakshi, stadi za ubunifu wa sauti na stadi zinazohusisha utendaji wa mwili.



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 106 15/04/2023 15:39

**Jedwali Na. 19: Kumudu Stadi za Kisanii, Ubunifu na Michezo**

| Kipengele | Kigezo | Kiashiria |
|---|---|---|
| **Sanaa** | Utendaji wa mikono | • Anabaini vitu vilivyomo katika mazingira<br>• Anaweza kuchora vitu, watu na wanyama<br>• Anaweza kuunda vitu |
| | Utendaji wa mwili | • Anafanya mazoezi ya kujenga mwili<br>• Anaweza kuunda vitu<br>• Anashiriki na wengine kufanya vitendo vya kujenga mwili |
| | Uimbaji wa nyimbo | • Anaweza kuimba nyimbo<br>• Anaweza kucheza ngonjera<br>• Anaweza kufanya majigambo |



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 107
15/04/2023 15:39

| Kipengele | Kigezo | Kiashiria |
|---|---|---|
| **Michezo** | Kucheza michezo na kujifunza | • Anaonesha urazini kutumia michezo katika kujifunza<br>• Anatumia michezo kujifunza<br>• Anaeleza namna ya kucheza<br>• Anashirikiana na wengine kucheza<br>• Anatenda matendo yanayohusisha utendaji wa macho na mikono<br>• Kuumba maumbo mbalimbali kwa mikono<br>• Kuunda vifani<br>• Kuimarisha/kutumia misuli ya mkono na vidole |



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 108
15/04/2023 15:39

## Umahiri wa Kutumia Dhana za Kihisabati

Dhana za kihisabati hutumika katika maisha ya kila siku ya mtoto. Dhana hizi zinahusisha uwezo wa mtoto kufikiri, kutenda na kutumia TEHAMA. Mtoto akijenga uwezo wa kuainisha vitu katika mazingira atakuwa na urazini wa kuyatumia mazingira yake katika ujifunzaji wa dhana za kihisabati. Mtoto hupimwa katika utendaji wa kutumia dhana mbalimbali za kihisabati kama vile, matendo ya kuhesabu vitu, kupanga na kuoanisha vitu, kutambua uhusiano wa vitu na namba, maumbo, dhana ya wakati, kumudu stadi za vipimo na kujenga dhana ya namba.

## Namna ya Kuumba/kuandika Namba

i. Mtoto aelekezwe namna ya kuumba/kuandika namba kwa kuzingatia ukaaji wake kama ni ya njiti tu mfano namba 1 na 7 au njiti na tumbo namba 6

ii. Hatua za uumbaji wa namba

    a. Kuandika michoro mama yenye kurahisisha uumbaji wa namba;

    b. Kuandika namba kwa kuzingatia hatua zake;

    c. Kuandika kwa usahihi; na

    d. Kuandika namba kwa kuzingatia unyanyuaji au kutonyanyua mkono.



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 109 15/04/2023 15:39

Namba zinazoandikwa kwa kutembeza mkono bila ya kunyanyua kiandikio wakati wa kuumba namba ambazo ni 0, 1, 2, 3, 6, 7, 8 na 9. Aidha, kuna namba ambazo huandikwa kwa kunyanyua mkono. Namba hizo ni 4 na 5



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 110 15/04/2023 15:39

**Jedwali Na. 20: Kumudu Stadi za Kutumia Stadi za Awali za Kihisabati, Kisayansi na TEHAMA**

| Kipengele | Kigezo | Kiashiria |
|---|---|---|
| **Kutumia stadi za awali za kihisabati** | Kuhusianisha vitu na namba | • Anataja vitu vilivyo ndani na nje ya darasa<br>• Anatofautisha vitu<br>• Anachora vitu |
| **Maumbo** | Kubaini maumbo | • Anabaini maumbo mbalimbali<br>• Anapanga maumbo kwa ruwaza<br>• Anachora maumbo<br>• Anahusianisha maumbo na rangi, pamoja na vitu<br>• Anabainisha vitu kulingana na sifa zake |
| **Vipimo** | Kutumia nyakati | • Anabainisha nyakati tofauti za siku<br>• Anabaini matukio kulingana na wakati |



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 111
15/04/2023 15:39

| Kipengele | Kigezo | Kiashiria |
|---|---|---|
| | | • Anataja siku za juma<br>• Anapima vitu mbalimbali<br>• Anaelezea vipimo |
| **Namba** | Kuhesabu namba | • Anaumba namba 1 - 10<br>• Anaoanisha namba na vitu kuanzia namba 1 hadi 20<br>• Anapunguza namba 1 hadi 20<br>• Anafanya hesabu nyepesi za mafumbo<br>• Anatamka namba 1 hadi 50<br>• Anapanga namba kwa mfuatano |



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 112 15/04/2023 15:39

### 3.3 Tathmini ya Ubora wa Shule

Upimaji wa matokeo ya ujifunzaji utafanyika kwa kutumia zana stahiki ambazo ni:

i. Fomu ya tathmini binafsi ya shule;

ii. Tathmini binafsi ya mwalimu;

iii. Uchunguzi darasani;

iv. Fomu ya matokeo ya ujifunzaji; na

v. Zana za upimaji wa ujifunzaji wa matokeo ya mtoto katika umahiri husika.

#### 3.3.1 Uchambuzi wa Taarifa za Upimaji na Uwekaji wa Kumbukumbu

Taarifa ya upimaji wa matokeo ya ujifunzaji baada ya kukusanywa kutoka shuleni zinatakiwa kuchambuliwa na kutafsiriwa baada ya kupitia taarifa kutokana na zana zote zilizotumika ili kupata taarifa halisi. Kwa mfano taarifa ya ujaribishaji wa zana hizi ilikusanywa kutoka kwa watoto 160 (wasichana 84 na wavulana 76) kwenye shule 80 katika mikoa ya Iringa, Morogoro, Mtwara, na Ruvuma.



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 113 15/04/2023 15:39

Tathmini ilikuwa modeli ambapo watoto walipimwa katika maeneo matatu tofauti ya umahiri ambayo ni utambuzi wa namba (kupitia Kifaa cha Upimaji cha Mtoto-Kuhesabu), kutambua herufi (kupitia Kifaa cha Upimaji cha Mtoto-Lugha na Mawasiliano) na kujenga hisia (kupitia Kifaa cha Upimaji wa Mtoto katika Vitendo vya Kuhusiana). Wapimaji walikuwa wakirekodi matendo ya watoto walipofanya vizuri, wastani au walioshindwa kwenye kazi ndogo tofauti kutoka maeneo matatu ambayo ni utambuzi wa namba, herufi na kujenga hisia.

Data ya kiasi pekee ilikusanywa kutoka kwa watoto na uchanganuzi wa kiasi ulitumika. Kwa kuwa data ilikusanywa kwa msingi wa karatasi, kulikuwa na mchakato wa kuingiza data katika majedwali na majedwali hayo yalionesha Nzuri (Vizuri), Wastani (Wastani), na ikiwa ameshindwa (Hajaweza) na grafu ilichorwa kudhihirisha matokeo katika picha.



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 114 15/04/2023 15:39

### 3.3.2 Mfumo wa Utoaji Taarifa za Matokeo ya Ujifunzaji wa Mtoto

Upimaji wa matokeo ya ujifunzaji wa mtoto utakuwa shirikishi, ambapo mfumo wa mawasiliano utafuata utaratibu uliopo. Taarifa za maendeleo ya mtoto shuleni zitatunzwa kwenye kanzidata ya shule. Kila ngazi ya utendaji itaweza kupata taarifa husika na kufanya maamuzi kutokana na changamoto itakayojitokeza ili kumwezesha mtoto kupata elimu bora.

## 3.4 Ziara ya Uthibiti Ubora wa Shule

Ziara ya uthibiti ubora wa shule itafanyika kwa siku mbili au tatu kulingana na ukubwa wa shule baada ya shule kujaza fomu ya kujitathmini yenyewe. Ziara itafanyika kwa kufuata hatua zinazofafanuliwa katika vipengele vifuatavyo:

### 3.4.1 Matayarisho Kabla ya Ziara

Kiongozi wa timu ya maafisa uthibiti ubora wa shule atatumia taarifa iliyotolewa na shule katika kujiandaa ili:

i. Kupata picha ya jumla ya utendaji wa karibuni wa shule na muktadha wake kama ilivyoelezwa kwenye fomu ya tathmini binafsi ya shule;

ii. Kupitia na kuchambua mpango uliopo wa utekelezaji na maendeleo;

iii. Kuandaa mpango wa kabla ya ziara na kuusambaza kwa wajumbe wengine ili:

   a. Kukumbushia na kusisitiza umuhimu wa kuzingatia kanuni na maadili wakati wote na kuchukua taarifa kwa usahihi na kufuata itifaki na taratibu zilizokubalika;

   b. Kugawa na kujadili majukumu ya kila mjumbe wa timu, kufuatana na sifa na uzoefu wa maafisa uthibiti ubora wa shule;

   c. Kukumbusha timu juu ya ufanyaji kazi ya tathmini;

   d. Kujitayarisha na kukubaliana maeneo ya ufuatiliaji na kuanza kuandaa maamuzi ya awali kila mwisho wa siku;

   e. Kusoma fomu ya mpango wa kabla ya ziara na kufanya rejea kwenye Mwongozo wa Uthibiti Ubora wa Shule ili kujiandaa na majukumu yao maalum wakati wakiwa kwenye eneo la kazi.



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 116 15/04/2023 15:39

### 3.4.2 Ziara Shuleni

Kiongozi wa timu ya uthibiti ubora akutane na mwalimu mkuu ili:

i. Kutambulisha timu na kusudi la ziara;

ii. Kutayarisha kikao na mwalimu mkuu;

iii. Kupanga ratiba kwa ajili ya mijadala ya vikundi vya watoto, wazazi/walezi, walimu na watumishi wengine;

iv. Kuthibitisha mpangilio wa utoaji mrejesho kwa walimu kufuatia mambo yaliyoonekana katika ufundishaji na ujifunzaji;

v. Kupata taarifa za watumishi waliopo na wasiokuwapo kazini au masuala mengine ambayo timu itapaswa kuyafahamu; na

vi. Kukutana na watumishi wote ili kutambulisha wajumbe wa timu ya uthibiti ubora wa shule na kuwaeleza kusudi la ziara yao.

Timu ya wathibiti ubora wa shule itajihusisha na shughuli za ufuatiliaji na tathmini ili kupata hali halisi ya namna shule/darasa la Elimu ya Awali linavyoendeshwa. Shughuli zifuatazo zitazingatiwa wakati wa ufuatiliaji na tathmini:

i. Ufundishaji na ujifunzaji ndani na nje ya darasa;

ii. Upimaji wa vitendo vya ujifunzaji wa watoto;

iii. Mapitio ya nyaraka zilizopo shuleni;



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 117 15/04/2023 15:39

iv. Majadiliano na wadau wa Elimu ya Awali katika shule/ darasa;

v. Kiongozi wa timu atatoa mrejesho wa kila siku kwa mwalimu mkuu kuhusu maendeleo ya ujifunzaji na ufundishaji; na

vi. Wathibiti ubora wa shule watakaa kikao kifupi cha kutoa maamuzi kwa kuzingatia ushahidi uliopatikana kwa lengo la kutoa mrejesho kwa wadau wote wa Elimu ya Awali shuleni.

### 3.4.3 Uandishi wa Taarifa

Timu ya wathibiti ubora wa shule itaandaa taarifa ya ufuatiliaji na tathmini na kuituma/kuisambaza kwa wadau mbalimbali.



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 118 15/04/2023 15:39

## SEHEMU YA NNE

## UFUATILIAJI NA TATHMINI YA UENDESHAJI WA ELIMU YA AWALI

### 4.1 Utangulizi

Ufuatiliaji na tathmini ya utoaji wa Elimu ya Awali utafanyika ili kupata taarifa ya utekelezaji wa Elimu ya Awali. Ufuatiliaji na tathmini utafanyika kupima ufanisi wa shughuli zote zinazofanyika kukidhi mahitaji ya mtoto katika nyanja za kiakili, kimwili, kijamii na kihisia ili kufikia utimilifu wake. Ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Elimu ya Awali utatumia mbinu zana na njia za ukusanyaji wa taarifa zitakazobainisha ni kwa kiasi gani viashiria vya ufanisi vimeweza kufikiwa.

Mchakato huu utafanyika kwa kuzingatia nyanja sita za ubora ambazo ni mafanikio ya mtoto, ujifunzaji na ufundishaji, ubora wa mtaala kukidhi mahitaji ya mtoto, uongozi na utawala, ushirikishwaji wa jamii na ubora wa mazingira ya shule na athari zake kwa ustawi, afya na usalama wa mtoto.



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 119 15/04/2023 15:39

## 4.2 Matokeo ya Tathmini ya Ubora

Matokeo ya tathmini ya ubora wa shule yatazingatia nyanja za mafanikio ambazo ni pamoja na mafanikio ya mtoto katika ufundishaji na ujifunzaji fanisi, ubora wa mtaala unaotekelezwa, uongozi na utawala wa shule/darasa, ubora wa mazingira ya shule, pamoja na ushirikishwaji wa jamii.

### 4.2.1 Mafanikio ya Mtoto

Mafanikio yanatafsiriwa kutokakana na utayari na ushiriki kikamilifu wa mtoto katika mchakato wa ujifunzaji na ufundishaji. Matokeo ya ujifunzaji wa mtoto yanatakiwa kupimwa kutokana na vitendo vya ujifunzaji ili kujua kiwango kilichofikiwa na kuweka kumbukumbu za mafanikio yake katika kanzidata.

**Matokeo ya Ujifunzaji wa Mtoto**

Mambo muhimu yanayotakiwa kuzingatiwa katika kubainisha matokeo ya ujifunzaji wa mtoto ni:

i. Kuchangamana na kushirikiana na wenzake;
ii. Kumudu stadi za maisha;
iii. Kumudu stadi za awali za kusoma, kuandika na kuhesabu;
iv. Kumudu stadi za utendaji unaohusisha viungo vya mwili na mikono;



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 120 15/04/2023 15:39

v. Kuwa na urazini wa kutunza mazingira; na

vi. Kumudu kutunza afya.

**Viashiria vya Mafanikio ya Ujifunzaji**

Upimaji wa matokeo ya ujifunzaji kwa mtoto wa Elimu ya Awali hufanywa kwa kuzingatia utendaji wa mtoto ili kubaini viashiria vinavyodhihirisha matokeo na maendeleo ya mtoto katika ukuaji na ujifunzaji. Kutokana na upimaji huo, changamoto mbalimbali zinazokwamisha ujifunzaji hubainishwa ili kutoa afua stahiki. Viashiria vya mafanikio ni pamoja na:

i. Taarifa za maendeleo ya mtoto kumudu kuchangamana na kushirikiana na wenzake;

ii. Taarifa zinazodhihirisha uwezo wa mtoto kumudu stadi za ubunifu;

iii. Kumbukumbu zinazodhihirisha mtoto kumudu stadi za maisha;

iv. Taarifa za maendeleo ya mtoto katika kujiheshimu na kuheshimu wengine;

v. Taarifa za maendeleo ya mtoto kuonesha uvumilivu na ustahimilivu;

vi. Kanzidata inayoodhihirisha kila mtoto alivyoweza kumudu stadi za awali za kusoma, kuandika na kuhesabu;



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 121 15/04/2023 15:39

vii. Shajara inayoonesha ni kwa kiwango gani mtoto amemudu stadi za utendaji unaohusisha viungo vya mwili na uratibu wa macho na mikono;

viii. Kumbukumbu zinazoonesha watoto kumudu vitendo vya urazini wa kutunza mazingira;

ix. Kumbukumbu zinazodhihirisha uwezo wa mtoto kumudu kutunza afya; na

x. Shajara inayoonesha ni kwa kiwango gani mtoto ameweza kuhimili maono yake.

### 4.2.2 Ujifunzaji na Ufundishaji

Mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji hupimwa kwa kuzingatia mahitaji ya mtoto.

**Ubora katika Ujifunzaji na Ufundishaji**

Ujifunzaji na ufundishaji unategemea zaidi umahiri wa mwalimu kumudu kuandaa mazingira ya ujifunzaji yanayomwezesha mtoto kuwa kiini cha ujifunzaji kwa kuzingatia mambo yafuatayo:

i. Mahitaji ya mtoto wakati wa ujifunzaji;

ii. Matumizi ya mbinu na njia zinazomshirikisha na kumhamasisha mtoto kujifunza;

iii. Utunzaji wa kumbukumbu za maendeleo ya upimaji wa kila mtoto;



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 122 15/04/2023 15:39

iv. Matumizi ya michezo kama mbinu kuu ya ujifunzaji na upimaji wa maendeleo ya mtoto;
v. Uchambuzi wa mtaala na vifaa vyake ili kuwezesha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wenye ufanisi;
vi. Uzingatiaji wa ratiba kuanzia kuwapokea watoto, mduara wa asubuhi, ufundishaji darasani, mduara wa mchana mpaka watoto wanaporudi nyumbani;
vii. Matumizi ya zana stahiki za upimaji wa matokeo ya ujifunzaji kwa kuzingatia umri, mahitaji ya mtoto na umahiri uliopendekezwa katika Muhtasari;
viii. Matumizi ya kona za ujifunzaji ili kumwezesha mtoto kushiriki kikamilifu katika ujifunzaji; na
ix. Matumizi ya zana stahiki za ufundishaji na ujifunzaji kulingana na muktadha wa ujifunzaji wa mtoto.

**Viashiria vya Ujifunzaji na Ufundishaji wenye Ufanisi:**

Kuna viashiria mbalimbali vinavyodhihirisha ujifunzaji na ufundishaji wenye ufanisi ambavyo ni:

i. Kumbukumbu za utekelezaji wa mtaala wa Elimu ya Awali na vifaa vyake, vikiwamo vya azimio la kazi, andalio la somo, shajara na nukuu za somo;
ii. Kumbukumbu za matokeo ya ujifunzaji;
iii. Mazingira ya ujifunzaji ndani na nje ya darasa yaliyoandaliwa vyema; na



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 123 15/04/2023 15:39

iv. Taarifa zinazobainisha matumizi ya mbinu na zana za ujifunzaji na ufundishaji kuwashirikisha watoto wote, wakiwamo wenye mahitaji maalumu.

### 4.2.3 Ubora wa Mtaala Unaotekelezwa

Ubora wa utekelezaji wa Mtaala wa Elimu ya Awali na vifaa vyake utafuatiliwa kubainisha viashiria pendekezwa kama vimefikiwa.

**Utekelezaji wa Mtaala Kukidhi Mahitaji ya Ujifunzaji wa Mtoto**

Mtaala wa Elimu ya Awali umeandaliwa kwa kuzingatia umahiri katika nyanja za ukuaji na ujifunzaji kiakili, kimwili, kijamii, kimaono, na kitabia. Utekelezaji wa mtaala na vifaa vyake unatakiwa uzingatie:

i. Mahitaji ya ujifunzaji;

ii. Sera ya elimu na mafunzo, sheria na kanuni zake;

iii. Maeneo ya ujifunzaji, umahiri na shughuli zinazotakiwa kutendwa na mtoto;

iv. Kukuza mahitaji ya kijamii kwa kuzingatia mabadiliko ya kiteknolojia;

v. Utunzaji wa kumbukumbu za shughuli za kila siku za mtoto;

vi. Uandaaji wa taarifa za uchambuzi wa vifaa vya mtaala kwa kuhusianisha ufundishaji na ujifunzaji;



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 124 15/04/2023 15:39

vii. Uchopekaji wa masuala mtambuko;
viii. Ufundishaji na upimaji kwa kutumia michezo ya utendaji kujenga dhana; na
ix. Kuwezesha utayari na ujifunzaji wa mtoto.

## Viashiria vya Utekelezaji wa Mtaala

Ili kuweza kupima utekelezaji wa mtaala, viashiria vifuatavyo havina budi kuonekana:

i. Nakala za Mtaala na Muhtasari unaotekelezwa;
ii. Mwongozo wa ufundishaji wa Elimu ya Awali;
iii. Vitabu vya kiada, ziada na rejea, vikiwamo vitabu vya hadithi;
iv. Machapisho yanayoendana na muktadha wa ujifunzaji;
v. Nukuu za kila umahiri na shajara zake;
vi. Kumbukumbu za matokeo ya ujifunzaji kwa kila mtoto;
vii. Nakala za maazimio ya kazi na maandalio ya walimu; na
viii. Nukuu za shughuli za watoto kutokana na umahiri husika.



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 125 15/04/2023 15:39

### 4.2.4 Ubora katika Uongozi na Usimamizi

Uongozi na usimamizi katika Elimu ya Awali unapaswa usimamie utekelezaji wa sera, sheria, kanuni, taratibu, na miongozo ya utoaji huduma stahiki kwa kuwashirikisha watoa huduma wengine, wakiwamo walimu, wazazi/walezi na jamii ili kuleta ufanisi wa utendaji kazi. Mambo muhimu ya kuzingatia ni pamoja na:

i. Uwapo wa Mpango wa Jumla wa Maendeleo ya Shule;

ii. Uwapo wa sheria ndogondogo na kanuni za shule zinazorejelea matakwa ya sera, sheria, kanuni, taratibu na miongozo inayohusiana na utekelezaji wa utoaji wa Elimu ya Awali;

iii. Kutoa mafunzo kabilishi ya Elimu ya Awali kwa wadau mbalimbali, wakiwamo walimu na walezi wanaohusika na utekelezaji wa Mtaala wa Elimu ya Awali;

iv. Kuandaa na kutunza kumbukumbu za kiutawala na nyaraka mbalimbali za Elimu ya Awali;

v. Kuzingatia kalenda ya shule inayokwenda sambamba na kalenda na miongozo ya utekelezaji wa mtaala wa Elimu ya Awali; na



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 126 15/04/2023 15:39

vi. Kutunza kumbukumbu za ushiriki wa jamii katika kutoa huduma stahiki za watoto pamoja na mahudhurio yao; na
vii. Kutumia kumbukumbu za ushiriki wa jamii katika kutoa huduma stahiki za watoto pamoja na mahudhurio yao.

Katika ufuatiliaji wa uongozi na uendeshaji wa shule/darasa la Elimu ya Awali, viashiria vifuatavyo vitabainishwa:

i. Jalada la taarifa za walimu wa Elimu ya Awali;
ii. Taarifa za uandikishaji wa kila mtoto na maoteo yake;
iii. Asilimia ya walimu wanaoshiriki katika mafunzo endelevu kazini;
iv. Kumbukumbu za taarifa za maendeleo ya watoto;
v. Mpango wa Jumla wa Maendeleo ya Shule unaoonesha vipaumbele vya utekelezaji wa kila mwaka;
vi. Barua za ruhusa, ripoti na vyeti vya ushiriki wa mwalimu katika mafunzo kazini;
vii. Mpango wa mafunzo kazini kwa walimu, zikiwamo kumbukumbu za ushirikishwaji wa wazazi/walezi katika utoaji wa huduma stahiki;
viii. Mtaala na vifaa vyake pamoja na miongozo ya uendeshaji wa Elimu ya Awali;



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 127 15/04/2023 15:39

ix. Kumbukumbu za maazimio, maandalio, shajara na nukuu za somo;

x. Namba ya usajili wa shule na taarifa za tathmini ya shule; na

xi. Nakala za nyaraka muhimu zinazosaidia utekelezaji wa Elimu ya Awali.

### 4.2.5 Ushirikishwaji wa Jamii katika Utoaji wa Elimu ya Awali

Ushirikishwaji wa jamii katika utoaji wa Elimu ya Awali ni nyenzo muhimu ya kuwezesha matokeo tarajiwa. Mambo muhimu ya kuzingatia ni pamoja na:

i. Kuhamasisha uandikishaji wa watoto waliofikia umri wa kujiunga na Elimu ya Awali;

ii. Kufanya utambuzi wa awali wa watoto wenye mahitaji maalumu na kutoa afua stahiki;

iii. Kushiriki shughuli mbalimbali za maendeleo ya ujifunzaji wa watoto; na

iv. Kupitia taarifa mbalimbali za utekelezaji wa malengo ya Elimu ya Awali.



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 128 15/04/2023 15:39

Katika ufuatiliaji wa ushirikishwaji wa wazazi/walezi, jamii na wadau wengine katika Elimu ya Awali, viashiria vifuatavyo vitabainishwa:

i. Mihtasari ya vikao na kumbukumbu za mahudhurio;

ii. Kumbukumbu za ushiriki wa wazazi/walezi katika maandalizi na utengenezaji wa zana za ujifunzaji na ufundishaji;

iii. Taarifa za maoni ya wazazi/walezi kuhusu ufuatiliaji wa maendeleo ya ufundishaji na ujifunzaji;

iv. Taarifa za ushiriki katika usimamizi wa tabia na mienendo ya watoto katika ujifunzaji;

v. Taarifa za vikao vya maamuzi katika masuala ya watoto kuhusu utoaji wa huduma stahiki;

vi. Kumbukumbu za uelimishaji wa jamii kuhusu umuhimu wa Elimu ya Awali; na

vii. Kanuni, taratibu, miongozo, machapisho, na kumbukumbu za utunzaji zinazohusiana na utoaji wa huduma ya chakula na lishe.

## 4.3 Viashiria vya Ufanisi

Ufanisi tarajiwa utapimwa kwa kuzingatia:

i. Umahiri wa timu fanisi ya uthibiti ubora wa ndani wa shule;



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 129 15/04/2023 15:39

ii. Matumizi ya taarifa za utekelezaji wa uthibiti ubora kwa maendeleo ya mtoto na shule kwa ujumla;
iii. Matumizi ya taarifa ya tathmini binafsi ya shule/darasa kutatua changamoto zilizobainishwa;
iv. Mrejesho kutokana na taarifa ya shule/darasa/kituo;
v. Mrejesho kutokana na taarifa za ujifunzaji wa mtoto; na
vi. Hatua zilizochukuliwa kuboresha utekelezaji wa Elimu ya Awali katika upatikanaji wa huduma na ujumuishaji, uchopekaji masuala mtambuka, taarifa za uthibiti ubora wa shule, uwekezaji katika Elimu ya Awali, uongozi, usimamizi, na uwajibikaji, na ufuatiliaji tathmini na utoaji wa mrejesho.



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 130 15/04/2023 15:39

## MAREJELEO


Anning, A., & Edwards, A. (2006). *Promoting Children's Learning from Birth to Five: Developing the New Early Years Professional.* UK: McGraw-Hill Education.

Bar-On, A. (2004). *Early Childhood Care and Education in Africa: The Case of Botswana. Journal of Early Childhood Research*. 2(1), 67- 84.

Berk, L E. (2005). *Infants and Children: Prenatal through Middle Childhood* (5th ed.). Boston: Pearson Education Inc.

Bhamani, S. (2017). *Educating Before Birth via Talking to the Baby in the Womb:* Prenatal Innovations Journal of Education and Educational Development Vol. 4 No. 2. pp 368 - 375.

Bodrova, E. & Leong, D. J. (2007). *Tools of the Mind: The Vygotskian Approach to Early Childhood Education*. New Jersey: Pearson Prentice Hall. (2nd ed.).

Hepper, P. (1991). *An examination of fetal learning before and after birth.* The Irish Journal of Psychology, 12(2), 95 - 107.




KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 131 15/04/2023 15:39

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (2013a). *Mwongozo wa Kuandaa na Kutumia Vifaa vya Michezo kwa Watoto Wadogo*. Programu ya Mafunzo Kazini kwa Walezi wa Vituo vya Kulelea Watoto Wadogo Mchana na Walimu wa Elimu ya Awali. Dar es Salaam: Wizara ya Elimu na Utamaduni

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (2013b). *Mwongozo wa Utambuzi wa Mapema wa Watoto Wenye Mahitaji Maalum na Afua Stahiki Umri (0 - 8).* Programu ya Mafunzo Kazini kwa Walezi wa Vituo vya Kulelea Watoto Wadogo Mchana na Walimu wa Elimu ya Awali. Dar es Salaam: Wizara ya Elimu na Ufundi.

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (2014). *Sera ya Elimu na Mafunzo.* Dar Es Salaam: Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Kleindorfer, S., & Robertson, J. (2013). *Learning before birth.* Australasian Science, 34(9), 27 - 32.

Mennella, J. A., Jagnow, C. P., & Beauchamp, G. K. (2001). *Prenatal and postnatal flavor learning by human infants.* Pediatrics, 107(6).

Mtandao wa Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Watoto Wadogo Tanzania (TECDEN). *(2013). Kiunzi cha Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto Tanzania.* Dar es Salaam: TECDEN.



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 132 15/04/2023 15:39

Naudeau, S., Kataoka, N., Valerio, A., Neuman, M. J. & Elder, L. K. (2010). *Investing in young children: An early childhood development guide for policy dialogue and project preparation.* Washington: The World Bank.

Paul, A. M. (2010). Origins: *How the Nine Months before Birth Shape the Rest of Our Lives.* New york: Simon and Schuster.

Selemani, H. (2016). *Malezi na Ujifunzaji Hatua ya I.* Dar Es Salaam: Education Press A.

Selemani, H. (2019). *Malezi na Ujifunzaji Hatua ya II.* Dar Es Salaam: Education Press A.

Skwarecki, B. (2013). Babies Learn to Recognize Words in the Womb. *Science Magazine*.

Smotherman, W. P., & Robinson, S. R. (1996). *The Development of Behavior before Birth.* Developmental Psychology, 32(3), 425-446.

Taasisi ya Elimu Tanzania (2015). *Muhtasari wa Elimu ya Msingi.* Dar Es Salaam: TET.

Taasisi ya Elimu Tanzania (2015). *Mtaala wa Elimu ya Msingi.* Dar Es Salaam: TET.



KUVEA ILIYOHARIRIWA 13 9 22.indd 133 15/04/2023 15:39

Taasisi ya Elimu Tanzania (2016). *Mtaala na Muhtasari wa Elimu ya Awali.* Dar Es Salaam: TET.

Taasisi ya Elimu Tanzania (2019). *Mwongozo wa Mwalimu wa Kufundishia Elimu ya Awali*. Dar Es Salaam: TET.

Tanzania Teachers' Union (2020). *Competence Profile for Early Childhood Education Teachers in Tanzania*. Dodoma: Tanzania Teachers Union.

*The Science of Early Childhood Development.* (2007): National Scientific Council on the Developing Child. http://www.developingchild.net

UNESCO. (2000). *Education for All: The Dakar Framework for Action*. Dakar, Senegal. Link http://www.unesco.org/education/efa/ed-for-all/framework.shtml

UNESCO. (2007). *EFA Global Monitoring Report: Strong Foundations – Early Childhood Care and Education*. Paris: UNESCO Publishing.

URT. (2013). Moduli ya Kwanza: *Ujuzi wa Malezi Changamshi kwa Watoto Wadogo.* TET. Dar es Salaam.

Yelland, N. (Ed.). (2005). *Critical Issues in Early Childhood Education*. Glasgow: Bell.